# Nipashe

Jumanne Mei 17, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580948

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



BREAKING NEWS

JACKPOT IMEPATA MSHINDI

TZS 1,255,316,060

SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#




## Waziri aagiza msako baba anayetuhumiwa kunajisi mtoto wake

UKURASA 4



## GUARDIOLA: LIVER NI TIMU BORA NILIYOWAHI KUIONA

UKURASA 21

# Mahakama yamaliza utata wa kina Mdee

UKURASA 2



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akitoa msimamo wa Bunge kuhusu wabunge waliofukuzwa uanachama na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) mjini Dodoma, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Wabunge wa kambi ya upinzani bungeni wakiwa kwenye kikao cha Bunge jijini Dodoma, jana. Licha ya kuvuliwa uanachama na chama chao bado wanahudhuria vikao hivyo kama kawaida. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Watumishi kikaangoni madai kughushi saini uhamisho

UKURASA 3



## Samia awakumbuka machinga, atoa mamilioni kuimarisha ofisi za mikoa

UKURASA 3


MICHEZO PABLO NA HESABU KUVUNA POINTI 21 UK.24

MAONI, KATUNI UK.6




Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe (kulia), akipokea kitabu kinachoelezea matumizi ya kidigitali kwa vyombo vya habari, kwa Mkurugenzi wa Taasisi ya WAN-IFRA Women in News Kanda ya Afrika, Jane Godia, alipotembelea ofisi za kampuni ya The Guardian Ltd, Mikocheni Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mahakama yaondoa utata

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania, Kanda ya Dar es Salaam imeamua wabunge 19 wa CHADEMA waliovuliwa uanachama waendelee kuwapo bungeni hadi maombi ya zuio la muda yatakaposikilizwa Juni 13, mwaka huu na kutolewa uamuzi.

Uamuzi huo ulitolewa jana na Jaji Mfawidhi John Mgeta wa Mahakama hiyo baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili.

Alisema hoja zilizowasilishwa ni nyingi na maombi yameletwa kwa hati ya dharura.

Pia alisema wabunge 19 wapo bungeni, waendelee kuwa bungeni hadi maombi yao yatakaposikilizwa na kutolewa uamuzi.

Alisema wajibu maombi watatakiwa kuwasilisha viapo kinzani mahakamani hapo kujibu mambo yaliyowasilishwa na waleta maombi.

Awali Wakili wa Halima Mdee na wenzake, Aliko Mwamanenge, aliomba mahakama itoe zuio la muda ambalo litawafanya waleta maombi wote kuendelea kushikilia nafasi zao bungeni kama wabunge wa viti maalumu.

"Tunaomba amri hii iendelee hadi tutakaposikilizwa maombi yetu kwa pande zote mbili na kutolewa maamuzi," alidai Mwamanenge.

Mjibu maombi, Wakili wa Serikali Mkuu, Gabriel Malata, alidai baada ya kutafakari tuhuma zilizotolewa na mjibu maombi namba mbili na tatu wanaiachia mahakama ione mazingira hayo kama yanawezesha Jaji kutoa amri hizo.

Pia aliomba wapatiwe muda na mahakama wa kupitia maombi yaliyowasilishwa ili waweze kujibu kiapo kinzani.

Mawakili wa CHADEMA, Peter Kibatala na Jeremia Mtobesya, waliwasilisha hoja sita za kupinga ombi la kutolewa kwa amri ya muda kutokana na upungufu katika maombi na viapo vya waleta maombi.

Akiwasilisha hoja hizo, Kibatala alidai kuwa katika hoja ya kwanza viapo vya waleta maombi sehemu moja wamesaini mawakili badala ya waleta maombi.

Alidai kuwa, pingamizi la pili hakuna kiapo kinachotaja dini zao, hamna kiapo kama dini, uhai wa kiapo ni maombi yenyewe.

Katika pingamizi la tatu, Kibatala alidai maombi yaliyowasilishwa hayajaonyesha kuwa yanataka nini na dhidi ya kina nani, amri ikitolewa itakuwa imetolewa dhidi ya nani na kwamba haitaeleweka.

"Amri za mahakama zinatakiwa ziwe zinaeleweka na kutekelezeka. Mheshimiwa Jaji haujaombwa, kwa hiyo hawawezi kutoa amri kwa sababu hakuna sehemu waliyokupeleka kufikia kutoa nafuu hizo," alidai Kibatala.

Pingamizi la nne, Kibatala anaeleza kuwa amri haiwezi kutolewa kwa sababu Bunge (Katibu wa Bunge) hayupo katika shauri hilo, wakati ofisi yao ndiyo inashughulikia masuala ya waleta maombi.

Kibatala anaendelea kuwasilisha mapingizi yake, kuwa katika pingamizi la tano Katiba inakataza suala lililofanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuchunguzwa.

Katika pingamizi la sita, hakuna sababu zozote zilizotolewa kuonyesha kwamba kuna hatari itatokea kama waleta maombi wakitolewa bungeni, "kwa hiyo jaji hajapewa hoja za kuthibitisha hiyo hatari."

Akijibu pingamizi hizo, Wakili Aliko aliiomba mahakama kutupilia hoja hizo na kuwapatia zuio la muda kama walivyoomba kwa sababu hoja walizotoa hazina mashiko.

Alidai, katika suala la viapo kutokuwa na dini sio suala la kisheria, kwa sababu mapingamizi yao sita kama walitaka kuyazungumzia walitakiwa kuwa na kiapo walichoapa kitakachokataa viapo vyao kuwa vina upungufu.

Halima Mdee na wenzake wamewasilisha maombi mawili Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam ya kibali cha kufungua kesi ya kupinga kuvuliwa uanachama na Baraza Kuu la CHADEMA, ambalo lilikaa Mei 12, 2022 na kufikia uamuzi huo baada ya kupigwa kura nyingi.

Maombi hayo yamefunguliwa dhidi ya bodi ya wadhamini ya CHADEMA, Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG).

Pia, wamefungua maombi ya zuio la muda (injunction) wakiomba waendelee kuwa wabunge hadi uamuzi wa maombi yao utakapotolewa.

# Msimamo wa Spika kuhusu wabunge 19

**Na Romana Mallya**

SPIKA wa Bunge, Tulia Ackson, amesema Bunge haliwezi kuingilia mchakato wa mahakama kuhusu hatima ya wabunge 19 wa Viti Maalum wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) mpaka uamuzi wa jambo hilo utolewe mahakamani.

Akizungumza jana bungeni jijini Dodoma, Spika aliwaeleza wabunge kuwa hayo ndiyo maelezo yake kuhusu jambo hilo linaloendelea ikiwa kutakuwa na maswali yoyote msemaji wa jambo hilo yeye.

**SAKATA LENYEWE**

Akizungumzia kuhusu suala hilo, Spika Ackson alisema kuwa usiku wa Mei 11, mwaka huu, kupitia mitandao ya kijamii walipata taarifa kuwa Baraza Kuu la CHADEMA limeazimia kukubaliana na uamuzi wa Kamati Kuu ya chama wa kuwafukuza wabunge 19 wa Viti Maalum.

Alisema Mei 12, mwaka huu saa 7:15 na dakika 38 mchana kwa njia ya barua pepe alipokea barua za wabunge hao 19 wakimfahamisha kuwa uamuzi uliofikiwa na Baraza Kuu CHADEMA la kuwavua uanachama kwa sababu ya vitendo vyao vya kuteuliwa na kukubali kuwa wabunge wa Bunge sio halali.

"Kuwa ni kinyume cha katiba na hayakuzingatia haki ya msingi ya kuwasikiliza ama kuruhusu kujitetea na kwa mantiki hiyo wabunge wao wamepinga uamuzi huo na mwenendo mzima wa uamuzi uliofanyika ndani ya chama katika Makahama Kuu ya Tanzania Dar es Salaam, kupitia shauri namba 16 la mwaka 2022 namba 16/2022 dhidi ya Baraza la Wadhamini wa CHADEMA, Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali," alibainisha.

Spika Ackson alisema tarehe hiyo hiyo saa 9:30 alasiri, Ofisa wa CHADEMA aliyejitambulisha kwa jina moja la Meshack alifika ofisi ndogo ya Bunge, Dar es Salaam kwa ajili ya kupeleka barua kwa Spika.

"Alipofika alielezwa na walinzi wa Bunge kuwa asubiri wafanye mawasiliano na kama wanaruhusiwa kupokea barua hiyo kwa kuwa wakati wa Bunge na maofisa wote wa ofisi ya Dar es Salaam huwa wanakuwa Dodoma.

"Wakati walinzi wanafanya mawasiliano hayo, ofisa huyo wa CHADEMA aliondoka bila kukabidhi barua hiyo na hii ni baada ya kupata maelekezo ya viongozi wa CHADEMA kwa simu kuwa wahusika hawawezi kupokea barua hiyo aondoke na watafanya utaratibu mwingine wa kuituma Dodoma."

Alisema ilipofika saa 9:15 na sekunde 24 mchana na saa 9:19 na sekunde 41 mchana kupitia barua pepe walipokea barua yenye kumbukumbu namba C/HQ/ADM/PARA/33/37 iliyotiwa saini na John Mnyika ambaye ni Katibu Mkuu wa CHADEMA.

Barua hiyo, alisema ilikuwa ikimjulisha kwamba katika kikao chake Mei 11, mwaka huu, Baraza Kuu la chama lilipokea na kujadili rufani za walioitwa waliokuwa wanachama 19 ambao walikata rufani dhidi ya uamuzi wa kamati kuu, Novemba 29, mwaka 2020.

"Na kwamba Baraza Kuu la chama hicho kwa mujibu wa ibara ya 7.7.12 (f) ya katiba ya chama hicho ya mwaka 2006 toleo la mwaka 2019, limeazimia kukubaliana na uamuzi wa Kamati Kuu ya CHADEMA wa Novemba 17, 2020.

"Hivyo waliokuwa wanachama wa CHADEMA wameendelea kukosa sifa za kudaiwa kuwa wabunge la Jamhuri ya Muungano Tanzania hivyo ni matumaini ya chama hicho kwamba itaufanyia kazi uamuzi wa Baraza Kuu la CHADEMA kwa mujibu wa katiba na sheria za nchi."

Spika alisema Mei 13, mwaka huu 2:42 asubuhi barua hiyo hiyo ilipelekwa kwa mkono ofisini kwake Dodoma na Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA, Singo Kigaila.

Pia, tarehe hiyo hiyo Mei saa 6:53 mchana barua hiyo iliwasilishwa tena kwake kwa njia ya DHL.

**MSIMAMO**

"Kwa mujibu wa katiba yetu mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano Tanzania ni mahakama, hivyo katika nchi yenye kuongozwa na msingi ya sheria na kuheshimiana kati ya mhimili mmoja na mwingine, Bunge haliwezi kuingilia mchakato wa mahakama na badala yake inalazimika kusubiri hadi hapo mahakama itakapotoa uamuzi wake kuhusu jambo hilo.

Alisema wabunge hao 19 walimtaarifu mapema Mei 12, mwaka huu kabla hajapokea taarifa yoyote rasmi kutoka CHADEMA kwamba wamekwenda mahakamani kwa ajili ya kulinda haki zao binafsi kama wanachama halali wa chama hicho na wabunge pamoja na kulinda katiba ya nchi na sheria ya taifa ya uchaguzi sura namba 343 iliyowafanya wao kuwa wabunge.

Alisema lazima wafahamu maelezo hayo yanatolewa kwa mujibu wa katiba, sheria walizozitunga Bunge.

"Hivyo, kwa kuzingatia misingi ya Katiba niliyoieleza ninalazimika kutotangaza kwamba nafasi za viti maalum vya wabunge 19 CHADEMA zipo wazi hadi hapo mahakama itakapokamilisha kazi yake ya kutoa uamuzi.

"Waheshimiwa wabunge hayo ndiyo maelezo yangu kuhusu jambo hili linaloendelea ikiwa kutakuwa na maswali yoyote msemaji wa jambo hili kuhusu wabunge hawa ni Spika."

Akitolea ufafanuzi kuhusiana na suala hilo wakati akizungumza na waandishi wa habari, Spika Tulia alisema Mahakama ikiwa na uamuzi wa jambo Fulani, mtu hawezi kusema hajui kwa sababu kesi ikifunguliwa, ni wajibu wa mtu kutafuta taarifa na si Mahakama kumwandikia muhusika.

# Watumishi kikaangoni madai kughushi saini uhamisho

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, ametoa siku tano kwa watumishi 12 walioghushi nyaraka za uhamisho mkoani Tanga kurudi kwenye vituo vyao vya kazi vya awali.

Sambamba na hilo, ameagiza watumishi hao wachukuliwe hatua za kinidhamu ikiwamo kurejesha gharama walizolipwa.

Bashungwa alitoa agizo hilo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapo huku akisema watumishi hao walihama kwa kughushi barua ambazo zilionyesha kama zimetiwa saini na ofisi yake.

"Naibu Katibu Mkuu Ramadhan Kailima, hili anza nalo umesema umeingia TAMISEMI kwenye treni inayotembea mwendokasi na wewe ni mzoefu. Hebu hili fuatilieni kuna watumishi takribani 12 walihama kwa kughushi barua kana kwamba zimesainiwa (zimetiwa saini) kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI," alisema.


Waziri alisema ndani ya siku tano watumishi hao wawe wamerudi kwenye vituo vyao vya kazi na kama kulikuwa na gharama zozote za kuwahamisha wazirudishe na mamlaka za nidhamu ziwashughulike ipasavyo kwa mujibu wa sheria na taratibu.

Katika hatua nyingine, Waziri Bashungwa amemwagiza Mkuu wa Wilaya ya Kilolo, Peres Magiri, kukaa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) kuja na njia sahihi ya kudhibiti uzito wa magari badala ya kuweka magoli ya mpira barabara.

"Kule Kilolo kuna jambo la ovyo, serikali imejenga barabara ya lami ya Kidabaga hadi Boma la Ng'ombe, jambo la ajabu wameweka magoli barabarani kudhibiti 'overload', lakini hawajui kuwa gari linaweza kubebea mzigo mkubwa wa mbao kavu na gari likipita kwenye mizani na likawa na uzito unaotakiwa," alisema.

"Lakini gari linaweza kubebea mzigo mdogo wa mbao mbichi na uzito wake ukawa ni mkubwa kuliko kiwango kinachotakiwa. Kusema ukweli haya magoli yaliyowekwa yanasumbua hata magari ambayo yanavyuma vya juu lakini hayana mzigo," aliongeza.

Alimtaka Mkuu wa Wilaya hiyo kutafuta njia sahihi ikiwamo ya kuwa na mizani inayohamishika.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akizungumza na Askofu wa Jimbo la Abu Dhabi, Mhashamu Askofu Paul Hinder ambaye ni mwakilishi wa Baba Mtakatifu katika nchi za Arabia ya Kusini baada ya kushiriki ibada katika Kanisa Kuu la Mtakatifu Joseph lililoko Mushriff – Abu Dhabi, Umoja wa Falme za Kiarabu jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# Rais Samia awakumbuka machinga

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema katika mwaka wa fedha unaoanza Julai mwaka huu, ofisi yake itatoa Sh. milioni 10 kwa kila mkoa kuwezesha shughuli za machinga nchini.

Rais Samia alibainisha hayo jana kwa njia ya simu baada ya kupiga moja kwa moja na kuzungumza na wamachinga waliohudhuria mkutano wa mafunzo ya viongozi wa Machinga nchini (SHIUMA).

Mafunzo hayo yanafanyika jijini hapo kwa siku tano yakihusisha viongozi wa Machinga Tanzania Bara na Visiwani.

"Nakushukuru Waziri kwa kuwapa machinga ofisi katika jengo la serikali, nimefuatilia risala yenu na nimefurahishwa nawahakikishia ushirikiano na mazingira mazuri na ifikapo mwaka wa fedha unaoanza mwezi Julai mwaka huu Ofisi ya Rais itatoa milioni 10, kwa kila mkoa kuwezesha shughuli za kuendesha ofisi za machinga mkoa," alisema Rais Samia.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alimpongeza Rais Samia kwa uamuzi huo ambao alisema umeleta tumaini jipya kwa machinga nchini.

Aliwataka machinga kuhakikisha kuwa fedha hizo haziwi chanzo cha kuvuruga umoja wao badala yake wazitumie kwa kazi iliyokusudiwa na kuwapo uwazi utakaoonyesha zimetumika kwa matumizi gani.

Pia, alimwagiza Katibu Mkuu wa wizara yake kuwakutanisha machinga na taasisi za fedha nchini ili kujadiliana namna ya kupunguza riba za mikopo kwa kundi hilo.

"Kama mheshimiwa Rais amewaahidi na kuwapatia kiasi hicho cha fedha kwanini taasisi za fedha zisione umuhimu wa kukaa meza moja na kundi hili kubwa ili kupunguza riba za mikopo na kuwawezesha mitaji," alisema Dk. Gwajima.

Kadhalika, alimwagiza Katibu Mkuu kufanya utafiti utakaosaidia serikali kujibu kero za kundi hilo badala ya kuendelea kufanya vitu kimazoea.

Vilevile, aliwataka machinga nchini kuhakikisha kuwa wanashiriki kikamilifu sensa ya watu na makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti 23, mwaka huu.

"Mnapaswa kujitokeza kuhesabiwa ili kuiwezesha serikali kupata takwimu sahihi tusiwe tunasema mpo milioni tatu kumbe mpo milioni sita hivyo wote mjitokeze kuhesabiwa," alisema.

Awali, Naibu Katibu Mkuu (SHIUMA), Joseph Mwanakijiji, alisema uhusiano mzuri walionao hivi sasa na serikali unasaidia machinga kuwa na mazingira mazuri na kufanya biashara kwa uhuru.

"Tuna changamoto nyingi, lakini kero ya miundombinu kwa baadhi ya masoko haiko sawa na kusababisha kiuchumi hatufikii malengo, baadhi ya miundombinu haiko sawa na kuhatarisha afya, ukosefu pia wa ofisi za machinga na changamoto za kibajeti," alisema.

Alizitaja changamoto nyingine kuwa ni pamoja na stadi za biashara, makazi bora, umilikishwaji wa maeneo ya machinga na kuomba kupewa barua ya idhini kuepuka kuondolewa mara kwa mara yanapotokea mabadiliko.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA U J E N Z I , UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA.

TANGAZO

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe 15.05.2022 hadi 29.05.2022 kampuni ya Spedag Interfreight itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka Holili kuelekea Moshi, gari hilo lenye namba za usajili:

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - Mita 21, Upana - Mita 4.3, Kimo -Mita 5.3**

3. Njia itakayotumika: Holili hadi Moshi kupitia Soweto, gari litasafiri muda wa mchana tu

**( Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

# Waziri aagiza msako baba anayedaiwa kumnajisi mtoto

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, ameagiza Jeshi la Polisi Mkoa wa Arusha, kumsaka Ally Abdallah, anayedaiwa kutoweka na mtoto wake wa kike wa miaka minne baada ya kumnajisi na kuharibika vibaya sehemu za siri.

Akizungumza jijini Arusha kwenye ofisi za Jeshi la Polisi, Dk. Gwajima alisema amefika mkoani hapo kwa ziara fupi ya uhamasishaji wa Siku ya Kimataifa ya Familia iliyofanyika Mei 15, mwaka huu.

Alisema akiwa katika ziara hiyo, alipata taarifa za kushtusha za mtoto huyo kunajisiwa na mama mzazi kuamua kumwachia Mungu, baada ya kwenda kwenye vyombo vya dola kutafuta haki ya mtoto wake.

"Kweli nilishtuka nikaamua kumfuata mama huyu eneo la Uswahilini jijini Arusha na nimeongea naye analia sana lakini nimewaambia wataalamu wa kisaikolojia wasaidie kwanza arudi kwenye hali yake," alisema.

Dk. Gwajima alisema inasikitisha kuona wakati nchi inajiandaa na maadhimisho ya siku hiyo, yenye kuhamasisha amani na upendo kwenye familia, kuna baadhi ya watu wamekutana na ukatili wa kijinsia na kuamua kumuachia Mungu badala ya kupeleka kwenye vyombo husika, jambo ambalo sio sahihi.

Dk. Gwajima alisema ni lazima haki za mtoto huyo zisikatiliwe, lazima zipatikane, hivyo kitendo cha baba japo mzazi kuondoka na mtoto akiwa katika hali hiyo, kumpeleka kwa mama wa kambo si sahihi.

Aliwaomba wananchi wanaokumbwa na matukio hayo, kwenda kwenye madawati ya jinsia au vituo vya mkono kwa mkono vilivyoko katika hospitali za mikoa kutoa taarifa ili wapate huduma stahili. Hata hivyo alisema kwa bahati mbaya tukio hilo tangu litokee Aprili 24, mwaka huu, halikufikishwa Polisi hadi Mei 12, mwaka huu, sababu ya kuamua kumwachia Mungu.

Kuhusu kilio cha mama mzazi wa mtoto huyo cha kuomba kusaidiwa kurudishiwa mtoto, kuwezeshwa kiuchumi na mahali pa kuishi, Dk. Gwajima aliagiza halmashauri impatie mkopo kupitia mikopo inayotolewa ili ajikwamue kiuchumi.

"Akijikwamua kiuchumi atapata mahali pa kuishi na yote yataisha,"alisisitiza.

Awali, akizungumza kwa uchungu mama wa mtoto huyo, Amina Abdallah (25), Mkazi wa Uswahilini jijini Arusha, alisema mtoto wake huyo alinajisiwa siku ya sikukuu ya Idd El Fitri. Alisema alitoka kwenda kucheza na wenzake jirani na nyumba yao na baada ya muda alirudi na pipi mkononi huku akiwa anatokwa damu sehemu za siri ambazo zilikuwa zinatiririka hadi miguuni.

"Baada ya kumuona mtoto wangu katika hali hiyo nilimuuliza kafanya nini akanijibu ameumizwa na kijiti. Nikamtishia nikamwambia usiponiambia ukweli nitajichoma kisu nife bado mtoto akazidi kusema amechomwa na kijiti," alisema.

Kutokana na majibu hayo, alisema alilazimika kumpeleka kwa majirani ili wamsaidie kumuuliza amepatwa na kitu gani lakini mtoto huyo hakusema chochote na ndipo wakaamua kumchapa kidogo akakojoa majimaji mazito meupe.

"Kutokana na maji hayo tulimkagua mtoto ndipo tukabaini kuwa amebakwa na kuharibiwa vibaya hali iliyotulazimu mimi na mama yangu mzazi na majirani kwenda kituo kidogo cha Polisi Uga Ltd na kupewa fomu namba tatu kisha tukenda Hospitali ya Rufani ya Mount Meru kwa ajili ya matibabu," alisema.

Alisema baada ya matibabu alirejea nyumbani ndipo baadhi ya ndugu na majirani wakamtaka asiendelee kumtafuta mhalifu aliyembaka mwanawe na kumshauri amwachie Mungu.

Alisema aliendelea kumuuguza mwanawe katika nyumba ya familia anayoishi yeye na mume wake pamoja na mama mkwe ambaye mahusiano yao siyo mazuri.

"Katika hali isiyokuwa ya kawaida siku ya Idd El Fitr mume wangu Ally Abdallah alimchukua mtoto wangu na kumpeleka kwa mke wake mdogo kijiji cha Sekano wilayani Kondoa kwa madai kuwa sijui kulea. Ninaomba serikali inisaidie ili niweze kurudishiwa mtoto wangu kwa sababu mume wangu aliondoka naye kimya kimya bila kunishirikisha," alisema.



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, akizungumza na Balozi wa Umoja wa Falme za Kiarabu nchini, Khalifa Abdulrahman Mohamed Al-Marzooqi, baada ya kusaini kitabu cha maombolezo katika ubalozi huo kufuatia kifo cha Rais wa Umoja wa Falme za Kiarabu, Sheikh Khalifa bin Zayed Al-Nahyan kilichotokea Mei 13, mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Bunge latangaza mabadiliko bajeti

**Na Romana Mallya,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Tulia Ackson, ametangaza mabadiliko ya ratiba ya kusomwa kwa Bajeti ya Serikali ambayo sasa itasomwa Juni 14 badala ya Juni 16, mwaka huu.

Aliyasema hayo jana bungeni jijini hapo kwamba kwa mwaka huu, kwa ajili ya bajeti ya 2022/23, nchi za Afrika Mashariki zimekubaliana kusoma bajeti Juni 14, mwaka huu. Alisema kutokana na mabadiliko hayo Mei 13, mwaka huu, Kamati ya Uongozi ilikutana na kufanya mabadiliko kwenye ratiba ya awali ambayo wabunge waligawiwa ikionyesha Bajeti ya Serikali ingesomwa Juni 16, mwaka huu, ambayo ni Alhamisi.

"Mabadiliko hayo yanaathiri siku ya bajeti na siku ya kupiga kura hapa ndani. Sababu ya mabadiliko hayo ni kwamba tunayo makubaliano nchi za Afrika Mashariki kusoma bajeti kwa siku moja.

"Kwa mwaka huu wa 2022 kwa ajili ya bajeti ya 2022/23, nchi za Afrika Mashariki zimekubaliana kusoma bajeti Juni 14. Tulipanga isomwe Juni 16, mwaka huu, hivyo inarudi siku mbili nyuma," alisema.

Spika alisema mabadiliko hayo pia yanaathiri makadirio ya mapato na matumizi ya kisekta kwa siku zilizokuwa zimepangiwa. Alisema makadirio yalikuwa yamepangiwa siku moja na mengine yalikuwa yaendelea hadi Juni 15, mwaka huu.

"Badala ya kusoma bajeti siku ya Alhamisi Juni 16, itasomwa Juni 14, mwaka huu. Tumezoea bajeti yetu husomwa Alhamisi, sasa haitakuwa Alhamsi bali itakuwa Jumanne, kwa hivyo Jumatano ambayo ni Juni 15, ni siku ambayo wabunge watapewa nafasi ya kusoma bajeti ili tuanze uchangiaji. Uchangiaji utaanza Juni 16 na Juni 15 itakuwa ya kujisomea," alisema.

Spika alisema tayari wizara mbalimbali zimetaarifiwa mabadiliko hayo pamoja na kamati za bunge ambazo zinatakiwa kuwasilisha taarifa zao sambamba na za wizara zinajiandaa vilivyo.

"Ni muhimu ifahamike kwamba tarehe ya kupiga kura imebadilika, hivyo itawataka wabunge wote wawapo Dodoma badala ya kupiga kura siku ya tarehe 28, iliyotajwa kwanza sasa kura itahitimishwa Juni 24, mwaka huu. Kila mbunge atatakiwa kuwapo bungeni kwa sababu utaratibu wa kura ya bajeti ni wa kura ya wazi na unaitwa jina moja baada ya lingine," alisema.

# Royal Tour yaleta watalii 796 kutoka Israel

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema kuzinduliwa kwa filamu ya 'Tanzania The Royal Tour', kumeanza kufungua milango ya utalii na kwamba watalii 796 kutoka Israel wameingia nchini.

Majaliwa aliyasema hayo juzi kwenye uzinduzi wa filamu hiyo mkoani hapa.

"Baada ya kuzinduliwa kwa filamu na kusambaa duniani, kwenye sekta ya utalii tumepokea watalii 796 walioingia nchini kutoka Israel ambao walikuja na ndege tatu zilizoandamana zenye uwezo wa kubeba abiria 262 kila moja," alisema.

Waziri Mkuu alisema hiyo ni faida ya Royal Tour na serikali inaendelea kufungua milango mbalimbali.

Alisema Watanzania wanapaswa kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuitangaza kwa bidii filamu hiyo yenye vivutio mbalimbali vilivyoko nchini.

"Ninawasihi Watanzania tusishawishike kudharau vya kwetu, tusimame pamoja kutangaza vivutio vyetu na kupitia utalii huu, tutafungua ajira kwa waongoza utalii na kada nyinginezo. Baada ya hapa, wana Dodoma twende tukaisemee filamu hii kwa kutumia simu zetu na mitandao ya kijamii," alisema.

Aliagiza wakuu wengine wa mikoa watenge siku moja na kuwashirikisha wananchi wao washuhudie kazi kubwa ambayo imefanywa na Rais.

"Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mheshimiwa (Anthony) Mtaka yeye kaanza. Ni vyema wakuu wengine wa mikoa watafute siku moja ya kuwaonyesha watu wao, wanaweza kuchagua hata kwenye ngazi ya halmashauri ili waone juhudi za Mheshimiwa Rais wetu," alisema.

Alisema kitendo cha Rais Samia kuruka kwa ndege na kuonyesha kwa karibu kilele cha Mlima Kilimanjaro, kimekata mzizi wa fitina juu ya mahali halisi uliko mlima huo.

Kuhusu fursa zilizoko Dodoma, Waziri Mkuu alitaja kilimo cha zabibu, usindikaji wa mvinyo, ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), eneo la kuandaa wapigania uhuru wa Namibia, Angola, Afrika Kusini, Zimbabwe na Msumbiji, mapori ya akiba ya wanyamapori ya Mkungunero na Swagaswaga na mazalio ya wanyama ya hifadhi ya Tarangire kama baadhi ya vitu vinavyoweza kuuinua mkoa huo.

"Uendelezaji wa vivutio hivi utawafanya wakazi wa Dodoma wapate mahali pa kupumzikia. Nawasihi wawekezaji waje Dodoma sababu ni mahali sahihi kwa uwekezaji na utalii.

Si hivyo tu, fimbo ya Mtemi Mazengo iko Dodoma, baiskeli yake aliyotumia iko Dodoma, kaburi lake liko Dodoma na pia nyumba ya kuhifadhi madini iliyojengwa mwaka 1925. Ninatoa wito kwa Bodi ya Utalii ishirikiane na uongozi wa Mkoa wa Dodoma ili kuhifadhi vivutio hivi," alisema.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbas alisema matarajio ya awali yalikuwa kuwafikia watu bilioni moja lakini kutokana na tafiti za kisasa, matarajio ya sasa ni kuwafikia watu bilioni mbili.

Alisema filamu ya Royal Tour ni fursa ya pekee ya kuitangaza Tanzania, ni fursa ya kutandaa duniani kwa kuwa Rais amekutana na wafanyabiashara maarufu na wamiliki maarufu wa kampuni mkubwa duniani ya utalii, filamu, meli za utalii na hoteli maarufu.

Awali, Mtaka alisema serikali ya Dodoma ina nafasi kubwa katika kuufanya mkoa wa Dodoma kuwa wa utalii nchini.

## HABARI KITAIFA

# Ummy ataja vipaumbele 13 afya 2022/23

**Na Romana Mallya**

WIZARA ya Afya imetenga Sh. trilioni 1.1 kwa ajili ya kutekeleza vipaumbele 13 ili kuboresha huduma za afya ikiwamo ujenzi wa hospitali maalumu ya mama na mtoto utakaogharimu Sh. bilioni 10.

Akiwasilisha jana bungeni Dodoma, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema kati ya fedha hizo za matumizi ya kawaida ni Sh. bilioni 554.3 na miradi ya maendeleo ni Sh. bilioni 555.13.

Ummy alivitaja vipaumbele hivyo kuwa ni kuimarisha utoaji wa huduma za chanjo kwa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano na kusimamia viwango vya ubora wa huduma za kinga na tiba katika ngazi zote za utoaji huduma za afya nchini.

"Tutawapima watoa huduma wetu katika hospitali zetu kuangalia ubora wa huduma, tutaangalia kwanza mgonjwa alivyofika katika kituo cha huduma alipata huduma nzuri ikiwamo kuchukuliwa historia yake, vipimo na dawa zote.

"Tutaangalia lugha na muda ambao mgonjwa ametumia katika kupata huduma za afya, tutasimamia ubora wa huduma za afya," alisema.

Alitaja eneo lingine kuwa ni kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, vifo vya watoto wachanga pamoja na mimba za utotoni.

"Tunakwenda kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa na vitendanishi katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya na kuimarisha huduma za lishe hususani kwa watoto wa umri wa chini ya miaka mitano, vijana balehe na wanawake wa umri wa kuzaa," alisema.

Vipaumbele vingine, kwa mujibu wa Waziri Ummy, ni kuimarisha huduma za afya na usafi wa mazingira ili kudhibiti magonjwa ya kuambukiza na hivyo kupunguza idadi ya wagonjwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini na kuimarisha miundombinu yake ikiwamo katika Hospitali za Rufani za Mikoa, Kanda, Maalum na Taifa.

Alitaja vipaumbele vingine ni kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi, kudhibiti magonjwa ya mlipuko, magonjwa ya kuambukiza na magonjwa yasiyo ya kuambukiza, kuimarisha utoaji wa mafunzo ya wataalamu katika sekta ya afya na kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini.

"Kuimarisha utawala bora



na uwajibikaji katika utoaji huduma za afya na kuimarisha mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na matumizi ya takwimu katika utoaji wa huduma za afya nchini.

Alisema wanataka pamoja na kujivunia majengo ya hospitali, vituo vya afya na zahanati waanze kusimamia namna huduma za afya zinavyotolewa kuanzia mgonjwa anavyoingia hospitalini mpaka anapopata huduma.

Waziri Ummy alisema ili kutekeleza vipaumbele hivyo, katika mwaka 2022/23, wizara imekadiria kutumia Sh. trilioni 1.1 kutekeleza majukumu ya wizara ikiwa ni pamoja na uendeshaji wa ofisi na miradi ya maendeleo.

Alitaja baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka 2022/23 ni kununua, kutunza, kusambaza na kutoa chanjo kwa watoto nchini ambapo kiasi cha Sh. bilioni 74. 4 zimetengwa.

Sh. bilioni 23.36, alisema zimetengwa kwa ajili ya kujenga vyumba vya huduma za watoto wachanga katika hospitali 100 za wilaya, kuwajengea uwezo watoa huduma kuwa na stadi, weledi na tabia bora katika kutoa huduma za mama na mtoto, kujenga, kuweka vifaa na watumishi wenye weledi kwenye ICU za wazazi katika hospitali za kanda na mikoa.

Alisema miradi mingine ni kuwezesha ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi na kuzisambaza katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya ambapo kiasi cha Sh. bilioni 200 zimetengwa na kukamilisha ujenzi wa hospitali tano za Rufani za Mikoa katika mikoa mipya ya Katavi, Geita, Njombe, Songwe na Simiyu ambapo jumla ya Sh. bilioni 18.6 zimetengwa.

Miradi mingine ni kukamilisha ujenzi wa hospitali mpya tatu za rufani za mikoa katika mikoa ya Shinyanga, Singida na Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Mara ambapo Sh. bilioni 26 zimetengwa na kuboresha huduma za matibabu ya ubingwa bobezi katika Hospitali ya Taifa na Kanda.

Alisema fedha hizo zitatumika kuimarisha miundombinu na ununuzi wa vifaa katika Taasisi ya JKCI, Hospitali za Rufani za Kanda za Chato, Mtwara, KCMC, Bugando, Mbeya na kuanza ujenzi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Magharibi.

"Kuimarisha Hospitali Teule ya Ukerewe ambapo Sh. bilioni 16.9 zimetengwa na kuendelea na ujenzi wa wodi ya wagonjwa binafsi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) Sh. bilioni 4 zimetengwa,"alisema.

Miradi mingine itakayotekelezwa mwaka 2022/23 alisema ni kuanza ujenzi wa jengo la kutolea huduma za uchunguzi na tiba ya saratani ikiwamo huduma ya mionzi katika Hospitali ya Benjamini Mkapa, Dodoma, Sh. bilioni 10 zimetengwa na kuendelea kukamilisha upanuzi wa miundombinu ya kutolea huduma za afya katika hospitali nane za rufani.

Hospitali hizo za rufani zitajengwa katika mikoa ambayo mikataba yake bado inaendelea ambazo ni Ligula (Mtwara), Tumbi (Pwani), Bombo (Tanga), Kagera, Maweni (Kigoma), Kitete (Tabora), Sekou - Toure (Mwanza) na Mawenzi (Kilimanjaro) ambapo kiasi cha Sh. bilioni 13.7 kimetengwa.

Kadhalika alisema wataendelea na ujenzi wa hospitali mbili mpya za mikoa ya Ruvuma na Sokoine (Lindi) ambapo Sh. bilioni 2 zimetengwa.

NMB Close to you

REQUEST FOR PROPOSAL (RFP)
PROCUREMENT OF VALUERS, QUANTITY SURVEYORS AND COLLATERAL MANAGERS FOR ZANZIBAR

1. NMB Bank PLC (the **"Bank"**) is a fully-fledged commercial bank listed at the Dar es Salaam Stock Exchange in Tanzania. The Bank offers banking services to individuals, small to medium sized businesses, large corporate clients, an government. NMB Bank has a wide distribution channel country wide that serves over 3.5 million customers.

2. The Bank is in need to procure Valuers, Quantity Surveyors and Collateral Managers for Zanzibar.

3. NMB Bank Plc now invites eligible, qualified, and experienced vendors to participate on the request for proposal for the procurement of ***Valuers, Quantity Surveyors and Collateral Managers***. This is strictly for Zanzibar based vendors and registered by governing professional bodies.

4. The selection and shortlisting of vendors will be conducted through the open competitive tendering as per the Bank's policy.

5. Interested and eligible vendors shall obtain RFP document from our website **www.nmbbank.co.tz/tenders** and request for clarifications on the RFP document shall be sent to the office of Secretary, Management Tender Committee at **procurement@nmbbank.co.tz** not later than (Friday 20th May, 2022).

6. The deadline for submission of proposals will be on Tuesday 31st May, 2022 at 1500 hours EA Time. Your proposal must be marked on the envelope/email: Procurement of Valuers, Quantity Surveyors and Collateral Managers (Please state the specific service you are applying for) and shall be delivered in either of the following ways: -
   - Hard Copy delivery in sealed envelopes and deposited at the **tender box located at NMB Bank Zanzibar branch, Malindi street, Stone town, Zanzibar**.
   - **Each service should have a separate application.**
   - Email delivery to – **tendersubmission@nmbbank.co.tz** (maximum document size 20MB)

7. Late tenders, portion of tenders, tenders not received, tenders not opened at the tender opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

**The Chief Executive Officer, NMB Bank Plc**
**NMB Head Office Ohio/Ali Hassan Mwinyi Street**
**P.O. Box 9213, Dar es Salaam, Tanzania, East Africa**

*www.nmbbank.co.tz*

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wananchi waandaliwe kufurahia matunda ya filamu ya Royal Tour

**WADAU** mbalimbali wanaeleza fursa zinazoibuliwa kuwapo kwa Filamu ya Royal Tour, ikiwamo umuhimu wa kufanya mabadiliko ya sheria na sera mbalimbali, ili kutoa kipaumbele kwenye sekta husika.

Jana Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alieleza kuwa matokeo ya filamu hiyo yameanza kuonekana na sasa wamepokelewa watalii zaidi ya 700 kutoka nchini Israel, tangu kuzinduliwa mwezi uliopita.

Aidha, Mwenyekiti wa Kamati ya Royal Tour, Dk. Hassan Abbas, alisema hadi jana habari za Royal Tour zimetangazwa kwenye vyombo vya habari zaidi ya 30 na kuwafikia watu milioni 546 duniani, huku 530 walisoma na kusambaza kwa wengine, jambo lililoendelea kuitangaza nchi sehemu mbalimbali.

Katibu Mkuu Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Prof. Godus Kahyarara, akizungumza kwenye mkutano wa mtandaoni kuhusu mafanikio ya filamu hiyo, alisema imesukuma mabadiliko ya sera na sheria ambazo zimepitwa na wakati.

Mathalani, alisema sera na sheria nyingi ni za miaka ya 90 ambayo haiko mbali na miaka ya 60, ambazo zilitambua kama kilimo ndicho kitatoa ajira na kukuza pato la nchi huku sekta ya utalii ikiachwa nyuma, hiyo ni kutokana na mazingira ya wakati huo.

Kwa sasa anasema wameona umuhimu kwa kufanya mabadiliko kwa kuwa nyingi zinashindwa kukidhi matakwa ya sasa na hilo limeonekana baada ya kuwapo kwa filamu hiyo na vikao vya mara kwa mara na wadau wa sekta binafsi.

Tunapongeza jitihada zinazofanywa kuhusu Royal Tour kwa kuwa zote zina lengo la kutangaza vivutio vilivyoko nchini duniani, ambavyo vitatembelewa na watalii ambao watatumia muda wao kuwapo nchini, mafanikio ikiwa ni kupata fedha za kigeni zaidi na ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja.

Vile vile, itasukuma kufungua fursa nyingine za utalii ambazo hazikuwa zinajulikana na zinaweza kuingiza fedha kwa nchi na mtu mmoja mmoja, kama ambavyo Zanzibar imejipanga kufungua utalii kwenye visiwa vya Pemba ambavyo visahaulika.

Ni muhimu serikali kushirikiana na wadu waliopo kwenye sekta ya utalii ambao ndiyo wamewekeza na wanafanya hivyo biashara ya kuuza huduma, ili kujua changamoto zilizopo na namna ya kuzitatua katika kujiandaa kupokea fursa zinazoletwa na filamu hiyo.

Kwenye utalii kinachouza ni huduma ambayo humfanya mgeni kutumia muda mwingi eneo fulani, ni muhimu kuwafundisha Watanzania namna ya kuyafikia masoko ya bidhaa hiyo duniani, kwa kuwa kumekuwa na madai kuwa kampuni zote kubwa za utalii zinamilikiwa na wageni na nyingi hazijafunguliwa nchini.

Kama ambavyo mwenyekiti wa maandalizi alivyoeleza kuwa Rais alikutana na wadau watano muhimu kwenye sekta ya utalii wakiwamo mawakala wa utalii duniani, mmiliki wa meli za kifahari, majumba ya kuonyesha filamu ambao wote wamejua kilichoko Tanzania na wanaweza kushawishi kutembelea.


Wapo waliokuwa wanaona filamu hiyo haigusi maisha yao kwa namna yoyote, lakini kwa matokeo ya awali yanaonyesha neema kwa nchi ambazo wananchi wanatakiwa kunufaika nazo, maana yake sekta binafsi na wadau wengine wanatakiwa kuwafikia wananchi ili wazione fursa muhimu. Mathalani, kwenye utalii kuna huduma nyingi zinazoweza kutolewa na wananchi wanaoishi jirani na hifadhi kama kuuza vyakula na bidhaa nyingine, ni muhimu wakafundishwa namna ya kuzalisha zinazokidhi mahitaji ya soko husika.

Imekuwa kawaida bidhaa au vyakula kununuliwa nje ya eneo husika kwa madai kuwa wananchi hawazalishi kwa viwango vinavyotakiwa, hivyo tunaona ni muhimu wakaelimishwa kuziona fursa na kuzitumia kwa kuwaeleza soko linataka nini.

Ndiyo wakati wa sekta zote muhimu ikiwamo kilimo kuwafikia wananchi kujua matakwa ya soko ili wanapolima wanajua ndicho kinachohitajika, kuliko kampuni za kitalii kuagiza bidhaa au vyakula kutoka nje na kupunguza ajira na fedha kwa mwananchi mmoja mmoja.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Bajeti elimu ifanikishe TEHAMA vijijini

Na Sabato Kasika

**MATUMIZI** ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) yanatajwa kuwa nyenzo muhimu kwa walimu na wanafunzi ili kuwaongezea uelewa zaidi kuhusu masuala ya teknolojia ya kidijitali madarasani.

Kutokana na umuhimu huo, kumekuwapo na juhudi mbalimbali za kuhakikisha watoto wanaanza shule ya msingi hadi vyuo vikuu wakiwa tayari wamefundishwa somo la TEHAMA.

Hata hivyo, pamoja na kuwapo kwa juhudi hizo, ufundishaji wa somo hilo unakwamishwa na changamoto ya ukosefu wa umeme kwenye baadhi ya shule, hasa za vijijini ambazo nyingi hazina nishati hiyo.

Serikali imejitahidi kupambana na mazingira hayo kwa kufanya kila liwezekanalo, ili kupata ufumbuzi wa changamoto hiyo, ili wanafunzi wote wa mijini au vijijini wapate fursa ya kujifunza somo hilo muhimu.

Tangu mwaka 2005 TEHAMA ilianzishwa kwenye mtaala mpya wa Elimu ya Msingi na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ili kumpa mwanafunzi maarifa na stadi za matumizi ya habari.

Lakini inawezekana ukosefu wa nishati kwenye baadhi ya shule ukawa kikwazo, kwani hata kama shule itakuwa na vifaa vya TEHAMA kama kompyuta wanafunzi hawawezi kujifunza somo hilo kwa vitendo kwa ukamilifu.

Ni imani yangu kuwa, kasi ya usambazaji umeme ikiongezeka, huku ikienda sambamba na uwapo kwa vifaa vya kufundisha somo hilo, ni wazi litawasaidia wanafunzi kuanzia mijini hadi vijijini.

Kwa kuwa ahadi ya serikali ni kwamba, hakuna kijiji kitakachoachwa bila umeme, basi ni vyema nishati hiyo ikaharakishwa kusambazwa kwa kasi iwezekanavyo ili kufanikisha ufundishaji wa TEHAMA.

Hilo likifanyika kwa ufanisi, wanafunzi wa shule za vijijini hawatabaki nyuma katika somo hilo, bali wote watakuwa wanakwenda kwenye uwiano na wenzao wa mijini katika uelewa unaolingana, kutokana na kujifunza kwa vitendo badala ya kubakia na nadharia zaidi.

Jitihada zinazofanywa na Wakala wa Umeme Vijijini (REA), ziwezeshe nishati hiyo kwenda shuleni badala ya kuishia katika nyumba za wanavijiji au katika maeneo ya biashara, shule nazo ziwe sehemu ya mradi huo.

Inawezekana idadi ya shule imeongezeka zaidi mijini na vijijini pia kupitia fedha za UVIKO-19, hivyo kila shule mpya kama ilivyokuwa ya zamani nayo inahitaji kipaumbele.

Hata hivyo, ni jukumu la bajeti ya Wizara ya Elimu iliyopitishwa wiki iliyopita kufanikisha upatikanaji umeme kwenye shule mpya na za kale ili kufikia hatima ya kufundisha TEHEMA nchi nzima.

Hayo yakifanyika, wanafunzi wa shule za vijijini hawatakuwa nyuma kwenye somo hilo huku wadau wa elimu nao wakishirikishwa ili kuhakikisha shule za huko zinakuwa na nishati na vifaa vya kufundishia somo hilo kwa tija na manufaa zaidi.

Wadau wa elimu wakishirikishwa, wanaweza kusaidia kupatikana kwa nishati hata ya sola na kompyuta kwenye shule hizo za pembezoni kwa kujitolea kuchangia fedha, vifaa na mafunzo au kununua vifaa hivyo ambavyo ni muhimu zama hizi za sayansi na teknolojia.

Njia hiyo pamoja na kuwajengea uwezo walimu wa somo hilo, kutokana na mabadiliko ya teknolojia ya mawasiliano duniani, wanaweza kufundisha kwa ukamilifu na hivyo kuwafanya wanafunzi kupiga hatua kwenye elimu na maarifa yatokanayo na kufahamu TEHAMA.

Hiyo ni njia mojawapo ya kuwapo kwa mazingira rafiki ya ufundishaji na ujifunzaji wa somo hilo kwa shule zote nchini, bila kujali kwamba ni za vijijini au mijini, kwani wanafunzi wote wanahitaji kufunzwa na kuelewa somo hilo lililopo kwenye mtaala.

Pamoja na hayo, ufundishaji wa TEHAMA kwa kutumia Kiswahili, ambayo ni njia bora, kwani lugha hiyo inasaidia kujenga saikolojia ya kujiamini na kujithamini na kujiongeza zaidi miongoni mwa wanafunzi.

# Mkurugenzi kortini madai kughushi saini na kujipatia mkopo mil. 350/-

**Na Maulid Mmbaga**

MMOJA wa Wakurugenzi wa Kampuni ya Mikocheni Shopping Mall, John Kyenkungu, amepandishwa mahakamani kwa tuhuma za kughushi saini na kujipatia Sh. milioni 350 kwa mkopo kupitia Benki ya Equity.

Kesi hiyo ya jinai imefikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu na kusikilizwa na Hakimu Mkazi Mwandamizi, Evodia Kyaruzi.

Wakati kesi hiyo ikisikilizwa Mei 12, mwaka huu katika mahakama hiyo, ilidaiwa kwamba Kyenkungu alighushi nyaraka na kuweka jina la Mkurugenzi mwenza, Said Nassoro na kwamba wamekubaliana kuchukua mkopo wa kiasi hicho cha fedha kutoka Equity Benki.

Katika shtaka la pili inadaiwa kwamba Kyenkungu alidanganya kwamba walikubaliana katika kikao cha Bodi ya Wakurugenzi wa kampuni hiyo kilichofanyika Julai 18, 2014 na kwamba mkurugenzi mwenzake Nassoro aliridhia kwa kuweka saini yake.

Nassoro ambaye ni shahidi wa kwanza alidai mahakamani kwamba alipata mshtuko baada ya kuona tangazo kwenye gazeti la Oktoba 18, 2019 kutoka Benki ya Equity ikitangaza kuuza eneo la Kampuni ya Mikocheni kwa madai ya kushindwa kulipa mkopo.

"Baada ya kuona tangazo hilo ilibidi nimuulize mkurugenzi mwenzangu Kyenkungu na alikiri kuchukua mkopo huo bila kinishirikisha," alidai.

Shahidi huyo alidai mahakamani kwamba alitoa taarifa polisi na kusababisha Kyenkungu kukamatwa na kuwekwa chini ya ulinzi na Jamhuri ilimfikisha mahakamani hapo baada ya uchunguzi.

Alidai kuwa hakuwahi kusaini nyaraka yoyote ya makubaliano ya kukopa pesa katika benki yoyote na wala kuhusishwa kwenye mazungumzo ya kutia saini.

Shahidi wa pili ambaye ni Mwanasheria wa Kampuni ya Lecal Link Attorneys Rainel Songea, alidai mahakamani jinsi alivyopelekewa nyaraka za benki za kuidhinisha mkopo na watu wawili waliojitambulisha kwa majina ya Kyenkungu na Nassoro na alidai kuwa watu hao waliweka saini mbele yake.

Alidai aliitwa polisi mwaka 2019 baada ya mlalamikaji Nassoro kulalamika kuwa nyaraka zilizokuwa na saini yake zilitumika kuchukua fedha benki kwa idhini ya saini yake.

Wakili huyo alidai mahakamani kuwa anamtambua Kyenkungu huku akidai kuwa Nassoro aliyekuwa naye siku ya kutiliana saini hakuwa katika mazingira ya mahakama na alishangaa kumuona mlalamikaji polisi akijitambulisha kwamba ndiye Nassoro ambaye ni tofauti na anayemtambua.

Kwa upande wa shahidi wa tatu ambaye ni Mwanasheria wa Benki ya Equity, Tumaini Lukumay, alidai kwamba walipokea nyaraka zilizokamilika kutoka kwa wakurugenzi wa kampuni hiyo ya kuridhia kuwa Kyenkungu apewe mkopo.

Pia, alidai kuwa taratibu za kisheria za kuchukua mkopo zilifuatwa, lakini baada ya mkopaji kushindwa kurudisha mkopo huo ambao ni pamoja na riba iliwabidi watangaze kuuza dhamana ya mkopo husika.

Mawakili wa Serikali katika kesi hiyo ni Tumaini Mafuru na Monika Ndakidemi huku mshtakiwa akitetewa na wakili wa kujitegemea Derick Kahigi.

Kesi hiyo inaendelea kusikilizwa mahakamani hapo.




Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Kilimanjaro (MECKI), Bahati Nyakiraria (aliyesimama), akieleza jana namna changamoto za kidijitali zinavyoilazimisha sekta hiyo hivi sasa kuingia katika mabadiliko. Katikati ni Mkuu wa Mkoa huo, Stephen Kagaigai. teknolojia. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Mbarawa asisitiza umuhimu wataalamu kujengewa uwezo

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amesisitiza umuhimu wa watumishi wa sekta ya ujenzi kujengewa uwezo na ujuzi katika utekelezaji na usimamizi wa miradi inayoendelea.

Kwa kufanya hivyo, amesema watawezeshwa kuendana na kasi ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia. Prof. Mbarawa alisema hayo mwishoni mwa wiki mjini Tabora, wakati akifungua mkutano wa baraza la wafanyakazi wa sekta hiyo.

Katika mkutano huo, pamoja na mambo mengine, alisisitiza umuhimu wa wataalamu wa usanifu wa barabara, madaraja na majengo kujiimarisha na kupata uzoefu ili kuboresha utendaji kazi na kupunguza gharama zinazoongezeka katika miradi kutokana na kukosewa kwa usanifu.

"Hakikisheni mnawapa ujuzi wa kutosha wataalamu wote ili waweze kuwa wabunifu, wanaojiamini na wenye uwezo mkubwa wa kusimamia miradi," alisema.

Waziri Mbarawa pia aliitaka wizara pamoja na Wakala wa Barabara (TANROADS), kusimamia kwa karibu malalamiko katika vituo vya mizani ili kuhakikisha mizani zote nchini zinakuwa katika ubora wakati wote na kutoa huduma nzuri kwa wadau wa usafirishaji.

Alisisitiza umuhimu wa watumishi wa sekta ya ujenzi kufanya mazoezi kila wakati ili kujiepusha na maradhi yasiyoambukizwa, hivyo kuwa na rasilimali watu kubwa yenye afya njema katika utekelezaji wa miradi.

Katibu Mkuu wa Wizara anayeshughulikia sekta ya ujenzi ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza hilo, Balozi Aisha Amour, alimhakikisha Mbarawa kuwa watumishi wa sekta hiyo wamejipanga kuhakikisha wanasimamia miradi yote ya ujenzi iliyopitishwa kwenye bajeti kikamilifu, hivyo kufikia malengo yaliyopangwa na wizara.

Balozi Amour alisema wamejipanga kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa wataalamu ili kuwajengea uwezo wa kuendana na mabadiliko ya mara kwa mara ya teknolojia na hivyo kuleta tija na ufanisi mahali pa kazi.

Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi Sekta ya Ujenzi pamoja na mambo mengine, umepitisha rasimu ya bajeti ya sekta hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/23.

# Viongozi wa mashirika waagizwa kutekeleza maagizo ya ukaguzi

**Na Mwandishi Maalumu**

MSAJILI wa Hazina, Mgonya Benedicto, amewataka watendaji wakuu wa taasisi, mashirika ya umma na wakala wa serikali kutekeleza kwa wakati mapendekezo yanayotolewa na wakaguzi wa ndani ili kudhibiti na kuondoa athari za vihatarishi katika taasisi wanazozisimamia.

Benedicto alitoa agizo hilo jana jijini Arusha kwenye ufunguzi wa mafunzo ya ukaguzi kwa kuzingatia vihatarishi (risk based audit) kwa wakaguzi wa ndani 474 kutoka katika taasisi, Wakala wa Serikali na Mashirika ya Umma 237 yaliyo chini ya Msajili wa Hazina.

Msajili alisema menejimenti ikisikiliza ushauri unaotolewa na wakaguzi, itaweza kuimarisha na kudhibiti mifumo ya ndani na kuondoa mianya ya ukiukwaji wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyowekwa, hivyo kuleta tija katika huduma na mrejesho wa uwekezaji unaotarajiwa serikalini. "Kunapokuwa na udhibiti wa ndani madhubuti, taasisi itafanya kazi zake kwa tija na kuwasilisha mapato yanayotarajiwa na kuwezesha serikali kutekeleza miradi mbalimbali iliyopangwa kufanyika, na pia kutoa huduma bora kwa wananchi," alisema Benedicto.

Pia aliwataka wakaguzi wa ndani ambao amewaeleza kuwa ndilo jicho katika taasisi na mashirika, kuyatilia maanani mafunzo hayo ili kwenda kuzisaidia taasisi wanazozikagua kwa kuwashauri juu ya kuimarisha udhibiti wa mifumo ya ndani.

"Ni imani yangu kwamba mafunzo haya yatawasaidia wakaguzi wa ndani wote watakaojengewa uwezo kwa kufuatilia na kutekeleza kwa ufanisi taratibu mbalimbali za ukaguzi na kuwashauri kwa makini maofisa masuuli ipasavyo," alisema.

Msajili alisema ofisi yake ambayo ina jukumu la kusimamia uwekezaji wa serikali na kuishauri kuhusu masuala ya uendeshaji na uwekezaji katika taasisi, mashirika ya umma, wakala wa serikali na kampuni ambazo serikali ni mbia, ilipanga mafunzo hayo kutokana na pendekezo la wakaguzi hao wakati wa mafunzo yaliyopita ya mfumo wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi yaani (GARI ITS) yaliyofanyika katika mwaka wa fedha wa 2020/21.

"Katika usimamizi wa taasisi, mashirika ya umma na wakala wa serikali, Ofisi ya Msajili wa Hazina imeona ni vyema iendeshe mafunzo yanayohusiana na ukaguzi wa kuzingatia vihatarishi kuwasaidia wakaguzi hao katika kuongeza uwezo wa utendaji kazi wao kiukaguzi na kuleta tija katika ushauri na mapendekezo wanayoyatoa kwenye taasisi zenu," alisema Msajili.

Aidha, Msajili aliwataka wakaguzi hao kuwaelimisha menejimenti juu ya kuzingatia vihatarishi na madhara yanayoweza kutokea iwapo vihatarishi havitazingatiwa na kudhibitiwa.

Msajili aliwapongeza wataalamu kutoka Ofisi ya Msajili wa Hazina wakishirikiana na Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuandaa mafunzo haya ambayo ni sehemu ya kuimarisha mifumo ya ndani ya udhibiti na usimamizi wa fedha za Umma katika Taasisi, Mashirika ya Umma na Wakala za Serikali.

Pia aliwashukuru wadau wa maendeleo wanaofadhili Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP) kwa kuwezesha kifedha kuhakikisha mafunzo hayo yanafanyika.

Naye Mkaguzi Mkuu wa Ndani, Magdalene Kirumba, akimkaribisha Msajili wa Hazina kufungua mafunzo hayo, alimshukuru kwa kutayarisha mafunzo hayo ambayo alisema ni muhimu kwa kuleta uelewa wa pamoja kuhusiana na dhana ya ukaguzi wa ndani kwenye mashirika ya umma.

Alisema mafunzo hayo yataboresha ubora wa taarifa za ukaguzi na kupunguza hoja za ukaguzi kwenye sekta ya umma.

Alisema pamoja na kuwapa maarifa mapya, wakaguzi lengo jingine la mafunzo hayo ni kujenga uwezo kwa wakaguzi wa ndani kuhusu miongozo ya kimataifa (International Professional Practice Framework -IPPF) na namna ya kutumia miongozo hiyo katika kufanya kaguzi mbalimbali.

# Maabara ya kisasa kufundishia wataalamu usingizi yazinduliwa

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu (MOI) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi za Afya Muhimbili (MUHAS), imezindua mradi wa maabara yenye vifaa vya kisasa vya kufundishia wanafunzi na wataalamu wa usingizi na ganzi.

Kuwapo kwa maabara hiyo nchini, kutasaidia kupunguza uhaba wa wataalamu ambao wanahitajika kwa uwiano wa 25 kwa wagonjwa 100,000 lakini nchini wako 75.

Mkuu wa Idara ya Usingizi na Ganzi wa MOI na Mratibu wa Mradi huo, Dk. Edwin Lugazia, akiwa katika hafla ya kuzindua mradi huo ulioko katika jengo la MOI, alisema utasaidia wanafunzi kujifunza kwa vitendo bila kuathiri maisha ya binadamu.

Alisema awali wanafunzi walikuwa wakijifunza kupitia wagonjwa ambao ikitokea wakakosea walikuwa wanahatarisha maisha yao.

"Lakini kwa mradi huu wanafunzi na wataalamu wetu ambao wataendelea kujinoa kupitia maabara hii, watakuwa na nafasi ya kukosea na kurekebisha makosa kwa kutumia mfano wa miili ya watu yenye hisia," alisema Dk. Lugazia.

Alisema mradi huo uko Afrika kwa lengo la kuongeza ufanisi wa wataalamu wa usingizi na ganzi kabla ya kufanyiwa upasuaji na baada ya upasuaji.

Kuhusu wataalamu wa usingizi na ganzi nchini, alisema uwiano uliopo haufiki mtaalamu mmoja kwa wagonjwa 100,000 hali ambayo inawafanya waendelee kuwezesha wanafunzi wengi kusoma masomo hayo.

"Lakini kwa Tanzania hata mtaalamu mmoja kwa wagonjwa 100,000 hata hafiki wakiwamo wapasuaji, wataalamu wa dawa za kinamama, upasuaji wa ajali, tuko mbali hata hatujafikia viwango," alisema.

Mtaalamu huyo alisema mpango huo utasaidia kupunguza wataalamu wengi zaidi kwa sababu Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC itaanza kufundisha ili kuwajengea uwezo kwa kutumia vifaa vya kisasa.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya MOI, Prof. Charles Mkony, alisema kuwapo kwa maabara hiyo kutasaidia wataalamu kujifunza kwa vitendo kwa kutumia vifaa hivyo vya kisasa ili kuondoa madhara kwa mgonjwa anayefanyiwa mafunzo kwa vitendo.

Alisema kutokana na maendeleo ya teknolojia yaliyopo wataalamu watajifunza kuendeleza ujuzi wao pamoja na wanafunzi wanaojifunza.

Naye Mwakilishi wa Makamu Mkuu wa MUHAS, Paschal Rugaria, alisema kwa kushirikiana MUHAS na MOI mafunzo ya wataalamu wa dawa za usingizi na ganzi watajifunza kwa vitendo.

Alisema idadi ya wataalamu wa dawa za usingizi na mahututi ni wachache ndio sababu ya MUHAS kuanzisha mitaala ya masomo hayo ili kupunguza upungufu huo nchini.

Kwa mujibu wa Rugaria, MUHAS inadahili wanafunzi 15 hadi 30 kila mwaka na inaendelea kutoa elimu kwa wanafunzi kusomea masomo hayo ili kupunguza upungufu uliopo.



Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, akimkabidhi hatimiliki Godfrey Mtewele mkazi wa Manispaa ya Iringa, wakati wa ugawaji wa hati kwa wananchi wa manispaa hiyo, kulia ni Kamishna Msaidizi wa Ardhi, Wenslaus Mtui, akishuhudia hivi karibuni. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Watu 100 kutolewa mtoto wa jicho

**Na Mary Geofrey**

MADAKTARI wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), kushirikiana na wa Korea, wanafanya upasuaji kwa watu 100 wenye tatizo la mtoto wa jicho.

Wataalamu hao wamekutana kwa ajili ya mafunzo yatakayofanyika kwa wiki mbili, yaliyoanza jana hadi Mei 27, mwaka huu na kuhusisha madaktari na wauguzi 12.

Akizungumza kwa Niaba ya Mkurugenzi wa MNH, Mkurugenzi wa Huduma za Upasuaji, Dk. Sufiani Baruani, jana hospitalini hapo, alisema mafunzo hayo yatakuwa na faida kubwa.

Alisema kwa upasuaji huo wa tundu dogo itafupisha muda wa mgonjwa kutibiwa kwa kuwa itapunguza gharama za kukaa hospitali.

Alisema ushirikiano kati yao na Korea ulianza mwaka 2016 kupitia Taasisi za Vision Care na Taasisi ya Kimataifa ya Ushirikiano wa Korea (KOICA). Kwa upande wake Daktari Bingwa wa Macho, Catherine Mapunja, alisema mafunzo hayo yatawasaidia kutumia njia za kisasa kulingana na ukuaji wa teknolojia.

"Njia hii ya upasuaji kwetu sio mpya, lakini vifaa vinavyotumika ni vipya hivyo tunajifunza, tunawashukuru kwani licha ya sisi kunufaika pia wagonjwa watanufaika," alibainisha.

Mkuu wa Idara ya Macho, Dk. Paul Nyaluke, alisema kuwa mtoto wa jicho ni tatizo la kutoona vizuri linalosababishwa na ukungu.

Tatizo hilo linasababisha kupata uoni hafifu na hata upofu kwa asilimia 40 hadi asilimia 50 nchini.

"Sababu ya tatizo hilo linaweza kuwa umri kuwa mkubwa, kuumia jicho, matatizo ya ugonjwa wa kisukari na anaweza kuzaliwa nayo kipindi mama akiwa mjamzito na akiambukizwa rubela au surua," alibainisha Dk. Nyaluke.

Naye Mkurugenzi wa Taasisi ya Vision Care, Dk. Kim Jaeyun, alisema wamekuwa wakishirikiana na nchi zingine za Afrika kama Ethiopia kwa miaka 10 na Uganda kwa kutoa mafunzo.

Alisema lengo lao ni kuwafikia asilimia 90 ya wataalamu wa afya ili kutoa huduma kwa ufasaha.

# Mwanafunzi wa chuo alivyofariki akiogelea

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

MWANAFUNZI wa Chuo cha Mifugo (LITA) mjini hapa zamani kikijulikana LITI, John Benako, amefariki dunia wakati akiogelea na wenzake wanne kwenye bwawa la Mambogo na mwili wake kuopolewa siku iliyofuata.

Tukio hilo ni la tano kujitokeza na kusababisha serikali kupiga marufuku utalii kwenye vyanzo vya maji.

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Wakili Albert Msando, amepiga marufuku kwa kusitisha shughuli zozote za utalii katika vyanzo vya maji ikiwamo katika Mto Morogoro, Milima ya Uluguru na maeneo mengine ya vyanzo vya maji, hadi utaratibu mwingine utakapotolewa baada ya kujiridhisha na shughuli za kiusalama.

Tukio hilo limetokea Mei 15, mwaka huu na mwili wa mwanafunzi huyo kuopolewa Mei 16, tukio jingine liliripotiwa mwezi uliopita la mwanafunzi wa Chuo Kikuu Mzumbe kwa kuangukiwa na jiwe kwenye Milima ya Uluguru wakiwa kwenye shughuli za utalii.

"Mwanafunzi Benako alikwenda na wenzake saba maeneo hayo kwa shughuli za utalii na wakaingia wanne kwenye maji kuogolea, lakini kwa kutofahamu mazingira, na ugeni wa lile eneo, inaonekana akaingia kwenye kina cha maji na kuzama ambapo juhudi za kutafuta mwili wake zilifanyika bila mafanikio siku ya kwanza, hadi siku ya pili alipoibuliwa na askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji," alisema Msando.

Akamwagiza Mkurugenzi wa Bonde la Maji la Wami-Ruvu kusimamia maelekezo hayo ya kuzuia wananchi kufanya utalii katika maeneo hayo hadi pale Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya itakapoweka utaratibu mzuri wakijiridhisha na usalama wa watumiaji wa maeneo hayo ili kuepusha matukio ya watu kufa maji ambayo huenda yakawa ni zaidi hata ya hayo matano yaliyoripotiwa rasmi.

Wakili Msando aliwataka wenyeviti wa serikali za vijiji, watendaji kata kusimamia agizo hilo mpaka pale watakaporuhusu kufanyika shughuli za utalii kwa utaratibu mzuri utakaowekwa wa kuhakikisha vyanzo vya maji vinalindwa na usalama wa maisha ya watu.

Mkurugenzi wa Bonde la Wami-Ruvu, Mhandisi Elibariki Mmasi, aliahidi kusimamia vyema maagizo hayo ya mkuu wa wilaya na kuonya watu wote watakaokiuka maagizo hayo.

"Maeneo haya yamekuwa yakitumiwa zaidi kwa shughuli za utalii na wakati wa matukio sherehe mbalimbali, licha ya kuwa hatari kwa wananchi, lakini yanatishia pia vyanzo vya maji," alisema Mhandisi Mmasi.

Aliwataka pia watu wanaochimba mashimo kwa shughuli za ujenzi kuyafukia baada ya matumizi ili kuondoa hatari zozote zinazoweza kujitokeza ikiwamo watu kufa maji hasa wakati wa mvua.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Morogoro, Emmanuel Ochieng, alisema walipata taarifa majira ya saa 9:45 alasiri na baada ya kufika eneo la tukio walianza kusoma mazingira na kuanza kumtafuta hadi walipositisha saa 12 jioni baada ya kumkosa.

"Siku ya pili tulianza kazi ya kutafuta mwili upya kwa kuomba mawazo ya wazee wanaofahamu vyema maeneo yale ambapo kati ya saa tatu hadi saa nne asubuhi mwili wa kijana huyo tuliuopoa na kuupeleka katika chumba cha kuhifadhia maiti cha Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro," alisema Ochieng.

# Shule zapata msaada taulo za kike

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SHULE za sekondari za serikali zipatazo 18 mkoani Njombe zimepatiwa katoni 2,600 za taulo za kike ambazo thamani yake ni zaidi ya Sh. milioni 83 ili kuwasaidia wanafunzi wa kike na kuachana na kutumia vitambaa.

Akizungumza jana wakati wa kukabidhi taulo hizo kwenye hafla iliyofanyika mjini hapa katika Shule ya Sekondari Mpechi, Meneja Mkuu wa Kampuni ya Mtewele Traders, Sady Mwang'onda, alisema kampuni hiyo kwa kushirikiana na Rospa International ya nchini Japan, wameamua kutoa taulo hizo ili kuwasaidia wanafunzi wa kike katika shule za sekondari mkoani hapa wanaokosa masomo kutokana na hedhi.

Mwang'onda alisema mtoto wa kike anapokuwa katika hedhi anaweza kukumbana na tatizo la kukosa ushiriki mzuri kwenye masomo yake kati ya siku tatu hadi tano kwa mwezi na kwa mwaka mzima anakuwa amekosa masomo kati ya siku 36 hadi 60.

Hata hivyo, alisema kwa kuona ukubwa wa tatizo hilo kampuni hiyo imeamua kuunga mkono jitihada za serikali kutoa taulo za kike kwa shule za sekondari za serikali mkoani Njombe ili wanafunzi hao wafanye vizuri kwenye masomo.

Alisema kitendo kilichofanyika cha kutoa taulo za kike ni moja ya kurudisha fadhila kwa jamii kutokana na shughuli ambazo kampuni hiyo inafanya ya uuzaji wa pembejeo za kilimo.

"Tukio hili la leo ni kubwa kwasababu linakwenda kugusa maisha ya kila mwanafunzi wa kike ambaye anasoma shule za sekondari za Mkoa wa Njombe," alisema Mwang'onda.

Ofisa Tarafa Wilaya ya Njombe Mjini, Lilian Nyemele, kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Njombe, alisema kupatikana kwa taulo hizo kunapaswa kuwafanya wanafunzi kuongeza bidii kwenye masomo kwa kuwa changamoto ya hedhi inapungua siku hadi siku. Alisema kwa kuzingatia uwapo wa wanafunzi wa kike katika shule mbalimbali, serikali imeendelea kuboresha miundombinu ili kupunguza tatizo hilo kwa wanafunzi wanapokuwa shuleni.

"Tusome kwa bidii tuache visingizio maana saa nyingine huumwi tumbo la hedhi, lakini unasingizia kisa umeona somo la hesabu," alisema Lilian.

Mwakilishi wa Ofisa Elimu Sekondari Halmashauri ya Mji Njombe, Augusta Wellah, alisema wanafunzi wapo wa makundi mbalimbali wanaoweza na kutumia taulo za kike na wengine ambao hawana uwezo kabisa.

"Serikali ina shule nyingi zenye wasichana wengi kwenye maeneo mbalimbali, lakini wameona waiunge mkono serikali kwa kuwapatia hawa watoto taulo za kike, tunawapongeza na kuwashukuru sana," alisema Augusta.

# Utoaji hatimiliki za kimila wamaliza migogoro ya ardhi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MPANGO wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), umetoa hatimiliki za kimila 2,625 na kumaliza migogoro ya wakulima na wafugaji na mgogoro wa ardhi katika vijiji mbalimbali vya Wilaya ya Mvomero.

Mtendaji Mkuu wa MKURABITA, Dk. Seraphia Mgembe, alisema hayo wakati akitoa taarifa kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu utekelezaji mradi wa urasimishaji ardhi na ujenzi wa Masijala ya Ardhi katika Kijiji cha Melela, wilayani Mvomero.

Alisema, migogoro hiyo imemalizika baada ya kupima mashamba 2,625 na kugawa hati za kimila kwa wananchi na kumaliza migogoro hiyo ya ardhi.

Alisema, MKURABITA kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, waliandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa makundi mbalimbali ambayo yanatumia ardhi ya kijiji.

Dk. Mgembe, alisema MKURABITA iliwezesha Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero kutoa mafunzo ya nadharia na vitendo ya kurasimisha ardhi kwa wataalamu wa ardhi na viongozi wa kata na vijiji ikiwa pamoja na kutoa vifaa vya upimaji wa ardhi kwa ajili ya utekelezaji.

Akizungumzia kuhusu ujenzi wa Masijala ya Ardhi katika Kijiji cha Melela, alisema MKURABITA imetoa Sh. milioni 47 kwa ajili ya ujenzi ili utunzaji wa hakimiliki za kimila za wananchi wanaorasimisha mashamba katika ngazi za vijiji.

Alisema pia ujenzi huo umewezesha uwapo wa ofisi ya kijiji kwa ajili ya kuendesha shughuli za kijiji kwa kuwa katika jengo hilo la Masijala ya ardhi pia kumetengwa vyumba kwa ajili ya ofisi ya mwenyekiti na ukumbi kwa ajili ya kuendesha mikutano.

Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Halima Okash, alisema wilaya hiyo ilikuwa inakabiliwa na migogoro mingi ya ardhi na wakulima na wafugaji, lakini baada ya kuingia mradi wa MKURABITA migogoro hiyo sasa imeanza kuisha na wananchi wanaendelea na shughuli zao za ujasiriamali.

Kwa upande wake, mmoja wa wananchi katika kijiji hicho, Abdallah Ally, aliiomba kamati hiyo kuwasaidia kupata hati zao za kimila kutokana na ofisi ya ardhi kuwazungusha na mpaka sasa waliopewa ni wachache.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, Abdallah Chaurembo, alitoa wiki mbili kwa uongozi wa Wilaya ya Mvomero kuwakabidhi wananchi hao hatimiliki zao za kimila.




Katibu Mkuu wa Chama cha ACT- Wazalendo, Ado Shaibu (kulia), akipokea zawadi kwa mmoja wa wanachama wa chama hicho, alipokuwa katika ziara ya uzinduzi wa mfumo wa kusajili wanachama kwa mtandao katika kata ya Zingiziwa jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wasiosafisha mashamba mikorosho kunyimwa pembejeo za bure

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WAKULIMA wa korosho wa mikoa ya Mtwara na Lindi ambao hawatasafisha mashamba yao kwa ajili ya upuliziaji wa mikorosho yao hawatapatiwa pembejeo za bure zinazotolewa na serikali.

Kauli hiyo ilitolewa jana wilayani hapo na Ofisa Kilimo wa Bodi ya Korosho Tanzania (CBT), Geofrey Mwalembe, alipokuwa akizungumza nao Kijiji cha Marika, kwenye mafunzo ya elimu ya matumizi sahihi ya viuatilifu vya korosho na usalama wa mabomba ya kupulizia.

Mafunzo hayo yametolewa na Taasisi ya Utafiti TARI Naendelee mkoani Mtwara na kuwakutanisha wakulima mbalimbali na wapuliziaji kutoka Wilaya ya Masasi.

Mwalembe alisema, mafunzo hayo yanalenga kumwandaa mkulima pamoja na wataalamu wa kilimo ili kutambua magonjwa mbalimbali yanayoathiri zao la korosho ili kukabiliana na magonjwa na wadudu wanaoharibu korosho.

Alisema kuwa utaratibu ulioletwa na serikali katika msimu huu wa 2022/2023 wa zao la korosho ni kutoa pembejeo za kilimo kwa wakulima.

"Tafiti zinaonyesha kwamba shamba ambalo limehudumiwa vizuri ikiwamo kusafishwa na kupuliziwa kwa kuzingatia elimu sahihi ya viautilifu linakuwa na uwezo mkubwa wa uzalishaji kuliko shamba ambalo halijasafishwa hivyo mafunzo haya yatasaidia kuongeza uzalishaji wa korosho," alisema.

Alisema, mafunzo hayo kwa wakulima na wataalamu hao yatakuwa chachu katika kutimiza lengo la Bodi ya Korosho katika uzalishaji wa zao hilo ambao ni uchumi wa kijani hasa katika mikao ya Mtwara na Lindi.

Alisema kuwa Bodi ya Korosho Tanzania imejiwekea malengo ya kupuliza tani za korosho 700,000 ifikapo mwaka 2025/2026 na katika msimu unaoenda wa mwaka 2022/2023 imeshaweka lengo la kuzalisha tani 400,000.

Mwalembe alieleza kwamba kupitia mipango na mikakati waliyojiwekea kama vile kutoa mafunzo kwa wataalamu wa kilimo, kuanzia kampeni ya kufufua mashamba na kutoa elimu sahihi ya matumizi ya viuatilifu vya mikorosho.

Hata hivyo, alisema serikali inatoa rai kwa wakulima wasiosafisha mashamba yao hawatapatiwa pembejeo hizo msimu huu.

Baadhi ya wataalamu waliopatiwa mafunzo hayo wameipongeza CBT na Taasisi ya utafiti TARI Naliendelee Mkoa wa Mtwara kwa kuwapatia mafunzo hayo kwa kuwa wamejifunza vitu vipya ambavyo awali walikuwa hawavijui.

Zakaria Hamisi mshiriki wa mafunzo ambaye ni mpuliziaji alisema mafunzo yamemsaidia kujua namna bora ya upuliziaji pamoja na kutambua kuchanganya viuatilifu kabla ya kuanza kupulizia.

Naye Abdallah Haridi kutoka Kata ya Chikukwe, alisema awali alikuwa akupulizia mikorosho bila ya kuwa na elimu kwa sasa ametambua namna ya mikorosho inavyotakiwa kupuliziwa hususani katika matumizi sahihi ya dawa ya mikorosho.

# Serikali yapunguza deni wanalodaiwa ATCL

SERIKALI imelipa Sh. bilioni 127.07 kati ya Sh. bilioni 141.77 zinazodaiwa na watoa huduma mbalimbali kwa Shirika la Ndege nchini (ATCL).

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, alibainisha hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Shaurimoyo (CCM), Ali Juma Mohamed.

Alihoji lini ATCL imeanza kulipa madeni ya kampuni zilizotoa huduma mbalimbali.

Akijibu, Naibu Waziri alisema serikali imeendelea kulipa madeni ya kampuni zilizotoa huduma kwa ATCL baada ya kuyafanyia uhakiki.

"Mwaka 2016 kabla ya serikali kuanza utekelezaji wa mpango wa kuifufua ATCL, kampuni ilikuwa inadaiwa Sh. bilioni 141.77 na watoa huduma mbalimbali za ndani na nje. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2022 serikali ilikuwa imelipa madeni ya Sh. bilioni 127.07," alisema.

Alisema itaendelea kuiwezesha ATCL kulipa madeni yaliyobaki kulingana na uwezo wa kibajeti.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo aliuliza hivi sasa ATCL imeanza safari za kubeba mizigo kwa ajili ya kwenda China na kupitia Zanzibar. "Ndege ya Boeing- 787 inatumiwa kubeba mizigo na imeundwa kwa ajili ya kubeba abiria na mizigo na eneo kubwa ni la abiria, lakini sasa shirika linabeba mizigo bila abiria hamuoni ni kulitia hasara, na lini shirika litaanza safari zake kisiwa cha Pemba," alihoji.

Naibu waziri alijibu shirika litaanza safari za Pemba mwaka wa fedha ujao wa 2023/24.



Wabunge wa kambi ya upinzani bungeni wakiwa kwenye kikao cha Bunge jijini Dodoma, jana. Licha ya wabunge hao kuvuliwa uanachama na chama chao bado wanahudhuria vikao hivyo kama kawaida. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## SADC yaahidi fedha uandaaji ujenzi reli Mtwara-Mbaba bay

JUMUIYA ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) imeahidi kutoa kiasi cha Dola za Marekani milioni sita kwa lengo la kumgharamia mshauri elekezi kuandaa andiko la ujenzi wa njia ya reli ya Mtwara-Mbamba bay na matawi yake ya Liganga na Mchuchuma yenye urefu wa kilometa 1,000.

Utaratibu wa kupata fedha hizo unaendelea na kazi hiyo inatarajiwa kufanyika mwaka wa fedha 2022/23.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Namtumbo (CCM), Vita Kawawa.

Mbunge huyo alihoji mpango wa ujenzi wa reli ya Kusini kutoka Mtwara hadi Ruvuma na matawi yake ya Liganga na Mchuchuma umefikia wapi.

Naibu Waziri Mwakibete, alisema serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC) imekamilisha kazi ya upembuzi na usanifu wa awali kwa ajili ya ujenzi wa njia hiyo ya reli.

"Upembuzi uliofanyika ulipendekeza kuwa utekelezaji wa mradi huo ushirikishe sekta binafsi. Kwa sasa serikali inaendelea na taratibu za kumwajiri Mshauri Elekezi kwa ajili ya kuandaa andiko, makabrasha ya zabuni ili kumpata mwekezaji kwa utaratibu wa ubia baina ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP)," alisema.

Katika swali lake la nyongeza, mbunge huyo alisema mradi huo upo kwenye mpango wa maendeleo wa miaka mitano na kuhoji ucheleweshaji wa upatikanaji wa mwekezaji na kufanya mazungumzo makini ili utekelezaji uanze kwa haraka kwa muda uliopangwa.

Akijibu swali hilo, Mwakibete alisema mazungumzo yatakapokamilika mradi huo utaanza kutekelezwa.




Habari zote na Augusta Njoji

# Uhifadhi vidakio vya maji tisa wakamilika

BUNGE limeelezwa kuwa serikali imekamilisha uandaaji wa mipango ya muda mrefu wa kuhifadhi vidakio vya maji katika mabonde yote tisa nchini.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, alieleza hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Maryam Azan Mwinyi.

Mwinyi alitaka kujua lini serikali itakomesha shughuli za ukataji miti, kilimo na ujenzi karibu na vyanzo vya maji ili kulinda vyanzo vya maji.

Mahundi alisema serikali inatekeleza Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Namba 11 ya mwaka 2009.

"Katika mwaka wa fedha 2021/22, serikali imekamilisha uandaaji wa mipango ya muda mrefu wa kuhifadhi vidakio vya maji (Catchment Conservation Plans) katika mabonde yote tisa nchini," alisema.

Alisema mipango hiyo imeweka dira, vipaumbele na utaratibu mzuri wa utunzaji wa vyanzo vya maji katika maeneo ya vidakio vya maji na mipango hiyo itatekelezwa hadi mwaka 2035.

Alisema serikali katika kuhakikisha inakomesha shughuli za ukataji miti kilimo na ujenzi karibu na vyanzo vya maji, hadi sasa jumla ya vyanzo vya maji 191 vimewekewa mipaka ikiwa ni hatua za kuzuia shughuli za kibinadamu katika vyanzo hivyo.

Vile vile, alisema na vyanzo 44 vipo katika hatua ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali ili vilindwe kisheria.

"Jumuiya za watumia maji 162 zimeanzishwa katika maeneo ya vyanzo vya maji ili kuwashirikisha wananchi katika shughuli za utunzaji wa vyanzo vya mji," alisema.

Aidha, alisema katika mwaka wa fedha 2022/23 elimu ya utunzaji wa vyanzo vya maji itaendelea kutolewa kwa wananchi ili wafanye shughuli za kiuchumi katika maeneo ambayo hayana athari kwa vyanzo vya maji na mazingira kwa ujumla.





Ukurasa 13

Machungu petroli, dizeli yanapokolea janga uhaba wa kuni, mkaa latikisa...





Ukurasa 12

**TARI Mikocheni yaibua shangwe wakulima minazi**

Nipashe
# TESA
Jumanne Mei 17, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

ELIMU NA SABATO KASIKA

# Wadau: Inakuwaje ajira, mafunzo walimu kisiwe kipaumbele 2023?

AJIRA na mafunzo kazini kwa walimu ni kipaumbele cha kipekee kinachotajwa na wachambuzi wa bajeti ya Wizara ya Elimu, iliyowasilishwa bungeni hivi karibuni, wakishangaa kwanini serikali imekiweka kando.

Wanatoa ushauri huo wanapozungumza na Nipashe kuhusu bajeti ya wizara hiyo na kile ambacho wanadhani, ingefaa serikali ikitazame kwa jicho pana wakati wa kutekeleza miradi ya kufikia maendeleo ya elimu.

Gratian Mkobwa ni rais mstaafu wa Chama cha Walimu (CWT), anapochambua bajeti ya Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, inayotaja uboreshaji wa mitaala, elimu ya juu, mikopo ya elimu ya juu na utafiti kuwa maeneo ya umuhimu wa juu kuwa vipaumbele.

"Vipaumbele hivi ni sawa, lakini ni lazima tuweke nguvu katika ajira za walimu wengi zaidi 10,000 pekee hawatoshi bado pengo ni kubwa."

"Pamoja na kuwaajiri pia tuwape mafunzo. Kuna upungufu mkubwa wa walimu, shule zimepungukiwa na zaidi ya nusu ya walimu, hivyo waliopo wanabeba mzigo mkubwa" anasema Mkoba.

Anakumbusha kuwa licha ya kuongeza shule za msingi kutokana na fedha za UVIKO-19, na serikali kutangaza ajira ya walimu, ikumbukwe wapo waliostaafu, kufariki, kuacha kazi, kuumwa, kupewa majukumu mengine na hata kufukuzwa.

Anasema la muhimu ni kuchambua upungufu huo kuajiri



Katibu wa Chama cha Kutetea Haki na Maslahi ya Walimu (CHAKAMWATA), Meshack Kapange. **PICHA: MTANDAO**

na kuwapa mafunzo kuendana na wakati.

Anaongeza: "Niliwahi kwenda shule moja ya sekondari nikakuta ina mwalimu mmoja wa Hisabati aliyepangiwa kufundisha vipindi 80 kwa wiki. Mazingira kama hayo ni kumchosha."

"Lakini kuna suala la mbinu bora za ufundishaji ambalo nalo ni la muhimu, kwani tangu tubadili mwelekeo wa elimu yetu ambayo sasa inatoa maarifa na ujuzi inakuwaje walimu hawapewi mafunzo kuandana na wakati?" anahoji.

Anaongeza kuwa baadhi ya walimu hutoka vyuoni wakiwa na ujuzi unaoendana na walichojifunza hivyo wanahitaji elimu ya mabadiliko yanayojitokeza wakiwa kazini na kushauri wapewe mafunzo kazini kwa ajili ya kujiongezea maarifa .

"Pamoja na hayo, nipongeze wizara kwa mkakati wa kutaka kutoa elimu inayoendana na soko la ajira, kutokana na ukweli kwamba, wahitimu wa vyuo wamebakia kuzurura mitaani kutafuta kazi," anasema.

### KIZUNGUMKUTI MITAALA

Akizungumzia kipaumbele cha kuboresha mitaala, Katibu wa Chama cha Kutetea Haki na Maslahi ya Walimu (CHAKAMWATA), Meshack Kapange, anasema kama nchi inataka kuboresha elimu, kutunga mitaala kurejeshwe kwenye Taasisi ya Kukuza Mitaala.

Mwalimu Kapange anasema Taasisi ya Ukuzaji Mitaala na ya Elimu Tanzania zirejeshewe majukumu ya kuzalisha vifaa vya kufundishia na kujifunzia, ili kuendelea kuboresha elimu nchini.

"Ninaamini kwamba, utaratibu wa kuwapa watu binafsi jukumu la kutunga mitaala umesababisha ubora wa elimu kushuka, lakini lipo suala la utawala ambalo nalo ni changamoto nyingine,"anasema Kapange.

Anafafanua kuwa utawala wa walimu wa shule za msingi na sekondari unasimamiwa na wizara mbili ya TAMISEMI, huku vifaa vya kufundishia, sera, mitaala vipo Wizara ya Elimu.

"Lakini walimu ambao hukaa na wanafunzi na kuwafundisha hawashirikishwi katika mambo ya uboreshaji wa elimu. Kwa hiyo wito wangu ni kwamba, wakati wizara ikiwa na mikakati mbalimbali ya kuboresha elimu katika mwaka wa fedha wa 2022/2023, iangalie ushirikishwaji wa walimu, taasisi za kuboresha mitaala na kuandaa vifaa kutimiza majukumu yake," anasema.

### UWEKEZAJI UTAFITI

Wadau wanaozungumzia utafiti wanashauri kuwekeza fedha za kutosha kwenye utafiti badala ya kutegemea wageni kuwekeza kwenye eneo hilo.

Baadhi ya wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, majina tunayo wanasema kazi nyingi za kitafiti nchini kwenye kilimo, viwanda, ubunifu, teknolojia zinakwama kutokana na serikali kutoweka fedha.

"Zipo taasisi nyingi za kitafiti, kuna Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, COSTECH, SIDO, TIRDO, CARMATEC, TEMDO lakini kazi zake ziko wapi zikibadilisha maisha ya Watanzania mijini na vijijini? Tunataka kuona kazi za kitafiti zilizokwama zikipewa fedha na msukumo ili ziwafikie wananchi na kuleta mabadiliko." Anasema mhadhiri jina tunalo.

INAENDELEA UK.12

TEKNOLOJIA
NA GERALD KITABU

# TARI Mikocheni yaibua shangwe

## • Ni wakulima wa minazi, yawasambazia miche ya kisasa inayozaa nazi 100

TAASISI ya Kituo cha Utafiti wa Kilimo -TARI Mikocheni Dar es Salaam, imemaliza hofu ya kutoweka kilimo cha minazi nchini baada ya kutafiti, kugundua na kusambaza kwa wakulima mbegu mpya ya kisasa na himilivu ya East African Tall (EAT), inayozaa nazi takribani 100.

Kuzorota kilimo cha minazi nchini, kulianza miongo takribani mitatu iliyopita baada ya wakulima wa ukanda wa pwani waliokuwa wanalima zao hilo kulalamikia kilimo hicho kuathiriwa na magonjwa na upungufu wa mazao.

Miti ya minazi iliyokuwa inalimwa zamani ilikuwa inazaa kati ya nazi tano mpaka 18 wakati ya sasa inazaa matunda 30 hadi 90.

Hayo yanaelezwa na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini TARI, Dk. Geoffrey Mkamilo, wakati wa kugawa miche bora na ya kisasa aina ya East African Tall (EAT), kwa wakulima wa ukanda wa pwani kutoka mikoa ya Lindi, Tanga, Mtwara na Pwani.

Katika maeneo mengine ya ukanda huo, baadhi ya wakulima waling'oa minazi na kupanda mazao mengine yenye faida kutokana na sababu mbalimbali kama miti kuzeeka, ukame na magonjwa, anaongeza.

Anasema serikali inataka kuona zao hilo lenye manufaa mengi likirudi katika ubora wake na kuchangia vilivyo katika uchumi wa taifa na kipato cha wakulima.

Anasema nazi inachangia kupata mafuta ya kupikia pia ni zao la biashara kwa watu wengi hasa kinamama na vijana, huongeza afya na virutubisho pamoja na kuhifadhi mazingira.

"Zao hili ni muhimu. Kina mama na vijana wengi hususani wa mikoa ya pwani wanafanya biashara ya kuuza nazi. Wengine wanazitumia kupikia, vijana nao wamejiajiri kuuza madafu. Kwa hiyo ni lazima tuhakikishe tunaliendeleza kwa kugawa mbegu bora aina ya EAT," anasema.



Wakurugenzi wa TARI, Dk. Joseph Ndunguru (kushoto) wa Mikocheni, Mkurugenzi Mkuu, Dk. Geoffrey Mkamilo na Mratibu Dk. Fred Tairo, wakimkabidhi Asha Msangi wa Wilaya ya Mtama miche bora ya minazi aina ya EAT. **PICHA: GERALD KITABU**

> Juhudi hizo zinalenga pia kuwapatia kipato wananchi wengi wa maeneo hayo ya ukanda wa pwani.

Anawataka wakulima na wakazi wa mikoa ya pwani kuzingatia maelekezo ya watafiti ikiwamo kilimo bora, kuandaa mashamba kikamilifu, mapema na pia kuchukua mbegu bora kutoka TARI ili wasichukue ziizochakachuliwa na wauza mbegu ambao hawatambuliki.

Aidha, anazitaka halmashauri kuanzisha mashamba ya mfano na kutenga bajeti ya kutosha kuendeleza minazi hiyo katika maeneo yao.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti cha TARI Mikocheni, Dk. Joseph Ndunguru, anasema sababu kubwa ya kuweka juhudi kubwa katika kufufua zao hilo ni kuhakikisha upatikanaji wa mafuta ya kula nchini.

Hivi sasa nchi inapambana kupata mafuta ya kula ya kutosha. Tuna upungufu wa mafuta hali inayosababisha taifa kutumia fedha nyingi kuyaagiza nje. Tunataka zao hili lichangie upatikanaji wa mafuta hayo," anasema.

Anaongeza kuwa juhudi hizo zinalenga pia kuwapatia kipato wananchi wengi wa maeneo hayo ya ukanda wa pwani.

Anasema kutuo cha ufafiti TARI Mikocheni kinagawa miche bora ili kubadilisha kilimo hicho kutoka kwenye kiwango cha kujikimu kwenda kwenye kilimo cha kibiashara. Anasema wananchi wana uwezo wa kupata mazao mengi na kuwekeza katika biashara za ndani na nje.

Akitolea mfano anasema mbali na kupata mafuta ya kupikia, wananchi wanaweza pia kuuza mbao au kutengeneza samani (fenicha) na kujipatia fedha.

"Kwa kushirikiana na halmashauri na serikali za mitaa tunataka kulifufua ili lianze kuzalishwa hata katika maeneo ambayo miche ya zamani ilikufa kutokana na changamoto mbalimbali," anasema Dk. Ndunguru.

Anaeleza kuwa kampeni hiyo imeanzia wilayani Pangani mkoa wa Tanga, na sasa inafanyika Mkuranga mkoa wa Pwani na Mtama mkoa wa Lindi.

Anasema katika wilaya hizo Kituo cha Utafiti wa Kilimo Mikocheni kitaanzisha vitalu ambavyo vitatunzwa na kuhudumiwa na halmashauri za wilaya kwa ajili ya wananchi wao.

Wakulima wanawake na vijana watatumia vikundi vidogo vidogo kuingia katika kilimo na biashara ya zao hilo.

Wakipokea mbegu hizo, wawakilishi wa Halmashauri za Wilaya za Mkuranga na Mtama, Julita Bulali na Asha Msangi wanashukuru serikali na TARI Mikocheni kwa mbegu hizo na kuongeza kuwa zitakuwa na tija kwa wakulima wa maeneo yao.

"Zao la minazi lilianza kutoweka taratibu na kipato cha wananchi kushuka kwa baadhi ya maeneo kutokana na sababu za magonjwa na ukame wa wastani. Wananchi wanayo furaha kubwa sana kupata miche bora," anasema Julita.

Anawataka wananchi wa Wilaya ya Mkuranga kuingia kwenye kilimo hicho hususani katika mnyororo wa thamani ili kupata fedha na kutunza mazingira yao.

Mwailishi wa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mtama mkoani Lindi Asha Msangi, anawataka wananchi kuchangamkia fursa hiyo ili kujipati kipato na kujiletea maendeleo.

TARI-Mikocheni ni moja kati ya vituo 17 vya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini, kilichoanzishwa kwa lengo la kufanya utafiti na kuendeleza minazi lakini kufanya majukumu mengine ya baioteknolojia.

# Wadau: Inakuwaje ajira, mafunzo walimu kisiwe kipaumbele 2023

INATOKA UK.11

**BAJETI YA 2022/23**

Katika mwaka wa fedha wa 2022/3, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imepanga kutumia Shilingi trilioni 1.49, huku ikiwa imeweka kipaumbele kwenye uboreshaji wa mitaala, elimu ya juu, mikopo ya elimu ya juu na utafiti, Waziri Mkenda anasema.

Anasema serikali imefanya tathmini ya mitaala 72 iliyowasilishwa na vyuo vikuu nchini na kutoa ithibati kwa mitaala hiyo na kwamba mingine 41 iko katika hatua mbalimbali za kupatiwa ithibati.

Lengo la kuboresha huduma ya mikopo hiyo ni kuwezesha wanafunzi wenye sifa na uhitaji kuendelea na elimu ya juu bila vikwazo.

**MIKAKATI YA WIZARA**

Kwa mujibu wa Profesa Mkenda, serikali itaendelea kuimarisha uwezo wa ndani wa kufanya utafiti na kutumia matokeo ya utafiti katika kuchangia ajenda ya maendeleo ya nchi.

Anasema, itafanya utafiti 252 katika maeneo ya mazingira, TEHAMA, nishati, kilimo na chakula, uongozi na biashara, maendeleo ya utalii, sheria, udhibiti wa ubora, utawala na maendeleo, watu wenye ulemavu na mahitaji maalum.

Prof. Mkenda anataja maeneo mengine ya utafiti kuwa ni maliasili, umaskini, utamaduni, haki za binadamu, maendeleo ya watu na mawasiliano, mifugo, biashara, uvuvi, elimu, sayansi, lugha na fasihi.

Kwenye suala la wabunifu, anafafanua kuwa serikali itawaibua, kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu na wagunduzi wachanga kupitia mashindano ya kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU), ili kuwezesha ubunifu wao kuchangia kikamilifu katika ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Walengwa wa ubunifu huo ni kuanzia shule za msingi na sekondari, vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi, vyuo vya ufundi, vyuo vikuu, vituo vya kuendeleza teknolojia, taasisi za utafiti na maendeleo pamoja na mfumo usio rasmi.

ELIMU
NA GAUDENSIA MNGUMI

# Machungu petroli, dizeli yanapokolea janga uhaba wa kuni, mkaa latikisa...

## • Ajabu tani 10 za miti, kuzalisha tani moja mkaa

INGAWA Tanzania ina utajiri mkubwa wa rasilimali za misitu na pengine muuzaji mkubwa wa mbao ghafi Afrika Mashariki, uhaba wa mkubwa wa mkaa na kuni kupikia majumbani na majiko ya biashara ni kitisho kinachokaribia kulikabili taifa.

Mchakato wa kupata nishati ya uhakika kwa ajili ya matumizi ya jikoni vijijini na mijini haujawa wa uhakika, hali inayodhoofisha juhudi za kufikia nishati endelevu kulinda mazingira.

Sekta ya nishati majumbani inayotumia kuni na mkaa imekuwa changamoto jijini Dar es Salaam na kutishia hatima ya familia nyingi.

Uchunguzi wa Nipashe umebaini kuwa licha ya bei za petroli, dizeli, mafuta ya taa na gesi kupaa kila mwezi, upatikanaji wa kuni na mkaa kupikia majumbani na migahawani nayo ni shida japo haijazungumzwa.

Malalamiko mengi ni ongezeko bei ya petroli na dizeli kupandisha gharama za kila kitu, sababu kubwa ikitajwa kuwa ni vita ya Urusi na Ukraine.

Licha ya gharama za kuni na mkaa zinazotumiwa na wakazi wengi mijini nazo zimekuwa juu kupindukia, lakini ni haba, mkaa ni wa miti michanga na myepesi inayogeuka majivu muda mfupi ikiwekwa kwenye jiko.

Kwa Dar es Salaam mkaa na kuni vinavyotumiwa kupikia ni haba na ghali kupindukia na familia nyingi zinatumia nishati isiyo rasmi kama vipande vya 'marine body' vinavyotumika kwenye ujenzi .

Zinapokaangwa chips na vyakula vingine uhaba unaonekana wajasiriamali wakijiongeza kwa kchanganya mkaa, kuni, makuti, makumbi na vifuu.

Sehemu nyingine kinamama na babalishe wanatumia vipande vya makasha ya mbao yaliyofungashia bidhaa mbalimbali zilizoingizwa nchini kutoka ng'ambo. Wapo pia wanaokusanya vipande vya mbao kutoka kwenye `saiti' zinazojengwa, vumbiranda,pumba za mchele.

### KUNI MKAA GHALI

Familia za kipato kidogo hutumia kuni hata miti ya mihogo na vinginevyo, wanavyoviokota mashambani.

Baadhi wananunua kuni sehemu unapouzwa mkaa, kipande kidogo pengine cha mwarobaini kikianzia shilingi 500 na kuendelea wakati mzigo wa vipande 10 unaweza kuzidi hata shilingi 5,000.

Baadhi ya mamalishe wa soko la Buguruni wanaozungumzia uhaba huo wanasema kuni ni ghali hasa zinapokuwa za miti migumu hufikia hata zaidi ya Shilingi 2,000 kwa kipande na hazipatikani.

"Wenzetu wanalalamikia mafuta ya pampu sisi hatuna wa kutusemea kuni na mkaa ni ghali mno. Kipimo kidogo cha mkaa ni Shilingi 2,000 hakiivishi maharage nusu kilo, " anasema mamalishe wa sokoni Buguruni.

Analalamikia: "Mkaa ni mwepesi mno labda wa matawi ya mwarobaini na mkurunge maana ndiyo miti iliyopo Dar. Miembe inapasuliwa mbao zinazotengeneza samani siyo kuchoma mkaa tena, sijui tunapoelekea..." anasema mjasiriamali huyo.



Uhaba wa mkaa na kuni unaongeza idadi kubwa ya wanaotumia makumbi na vifuu kupikia. **PICHA: MTANDAO**

### JANGA LA NISHATI

Wafanyabiashara wa kuni na mkaa wa maeneo ya Mbagala, Manzese na Buguruni, wanaamini miji mingi huenda inakabiliwa na uhaba mkubwa wa kuni na mkaa wakihofia ni tatizo la kitaifa.

Dkt. Felcian Kilahama, Mkurugenzi mstaafu wa Idara ya Misitu na Nyuki, anapoulizwa kuhusu hofu ya uhaba wa nishati hiyo anasema ni suala linalohitaji utafiti kujua ukweli.

Anakumbusha kuwa misitu imekuwa chanzo kikuu cha riziki kwa Watanzania wengi, nguzo kuu ya ustawi wa taifa kuanzia uhifadhi wa mazingira, kilimo, wanyamapori na utalii, uwiano kiikolojia na uzalishaji wa bidhaa na rasilimali muhimu kama mbao, kuni na mkaa au nishati lakini haijalindwa kikamilifu.

"Sekta ndogo ya misitu ya asili inahitaji kusimamiwa ipasavyo, inakosa ulinzi inaharibiwa na hii itachangia pakubwa katika ukosefu wa mikaa na kuni mijini na vijijini kama watu wanavyodai."

Anaeleza kuwa hata mkaa unaozalishwa leo ni wa miti michanga na kiwango cha kuni kinachouzwa na kuingizwa mijini ni kidogo na kinazidi kupungua.

Anasema juhudi zinahitajika na kukumbusha kuwa bila menejimenti na usimamizi madhubuti wa misitu ni muhimu na kwamba misitu ni mlinzi na mwendelezaji sekta zote zinazozalisha mapato na ajira nchini.

Anatoa mfano kuwa misitu ina umuhimu kwenye kilimo inaleta mvua, ni chanzo cha mvua na maua kwenye asali, ndiyo makao ya wanyama na viumbe pori, vyanzo vya maji, kusafisha hali ya hewa na kuondoa hewa ukaa angani. Aidha ni malighafi ya mbao kwenye ujenzi na karatasi, lakini ni chanzo cha nishati hasa kuni na mkaa zinazotumika nchini kote.

> Sekta ndogo ya misitu ya asili inahitaji kusimamiwa ipasavyo, inakosa ulinzi inaharibiwa na hii itachangia pakubwa katika ukosefu wa mikaa na kuni mijini na vijijini kama watu wanavyodai.

Mtaalamu huyo wa misitu anasema: "Mahitaji ya kuni na mkaa yanaelekea kupita uwezo wa uzalishaji, hivyo, uvunaji wa rasilimali za misitu kwa mahitaji ya nishati na ujenzi yalihitaji kupangwa na kusimamiwa vizuri kwani kuna hatari kwa mazingira."

### UVUNAJI Vs UPANDAJI

Dk. Kilahama anasema watu wanalalamikia ukosefu wa kuni na mkaa mijini, lakini Watanzania wengi wavuna zaidi kuliko kupanda kutumia kuni na mkaa kwa fujo kuliko kuwa waangalifu na wanaobana matumizi.

Anasema kwa mfano, ukifika vituo vikuu vya kupika vyakula kwenye barabara kuu wengi wanapika vyakula kwa mkaa mwingi, bila majiko banifu, tena wengine wakitumia majiko ya 'ringi za matairi' bila kujali kuwa mkaa na miti vinakaribia kutoweka kama ambavyo uoto wa asilia unavyomalizika.

"Nimefanya utafiti nikagundua kuwa wanatumia mkaa kwa fujo kwa sababu wanaupata pengine kwa njia zisizo rasmi kwa ujanja na gharama nafuu, hivyo hawaoni hasara, japo ni janga kwao na kwa taifa. Itafika siku hakuna miti wala mkaa na kuni wote tutaumia..." anaonya.

### MKAA NI HASARA

Anasema kama watu wanavyolalamikia kupungua mkaa mijini ni jambo ambalo lilifahamika kwa kuwa kuchoma mkaa kunamaliza miti na misitu.

"Ni wakati wa kuboresha matumizi ya kuni na kuachana na mkaa unaoleta hasara kubwa kwenye misitu ya asili na mifumo ya ikolojia, kwa mfano kuchoma tani 10 za miti ili kupata tani moja ya mkaa. Huo ni uharibifu mkubwa wa mazingira na maliasili miti," anaonya Dk. Kilahama.

Anasema licha ya kuwepo teknolojia ya uchomaji mkaa kisasa unaopunguza uharibifu lakini hata teknolojia hiyo ya kisasa zaidi haina manufaa kwa vile huchoma tani sita za miti kupata tani moja ya mkaa ambayo ni hasara pia.

Lakini, anasema vifaa vyake ni ghali na siyo wengi wanaoweza kumudu, akisema unatumia mapipa makubwa ya kuchoma

INAENDELEA UK.14

# Machungu petroli, dizeli yanapokolea janga uhaba wa kuni, mkaa latikisa...

INATOKA UK.13

mkaa yenye matanuru na mifuniko ambayo baada ya kujaza miti moto huwashwa, mifuniko hufungwa kuzuia hewa ya oksjeni kuiingia ndani ya tanuru.

Anaeleza kuwa mapipa hayo au 'wood retorts' yangeweza kutengenezwa nchini na kupiga marufuku uchomaji mkaa wa kizamani ambao unatishia hatima ya miti, misitu na mazingira.

### MAJIKO BANIFU YA KUNI

Dk. Kilahama anataka kuwekeza zaidi kutengeneza majiko banifu ya kuni, ambayo yataboresha muundo wa matumizi ya kuni ili zitumike kidogo kwa ufanisi mkubwa kupika chakula kingi kwa nishati kidogo zaidi.

Anasema majiko hayo yatumike nchi nzima ili kuokoa miti na misitu na kuhamasisha ulinzi wa misitu ya asili, upandaji kwa kasi kubwa wa miti ya asili pia kupunguza shughuli zinazotishia hatima ya sekta ya misitu.

Anakumbusha kuwa misitu ni mlinzi wa hali ya hewa na mdhibiti wa mabadiliko ya tabianchi, ndiyo mtoaji wa hewa safi, mlinzi wa bioanuwai za viumbe, maeneo ya maji, udongo, nishati na kilimo cha mazao ya chakula na utoaji wa vifaa vya ujenzi vya mbao na miti.



Magogo ya miti yakiwa yameandaliwa kwa ajili ya kuchomwa mkaa. Tani 10 za miti zinapochomwa huzalisha tani moja ya mkaa, mchakato unaoelezwa kuwa ni wa hasara, unaomaliza misitu na kuharibu mazingira. **PICHA: MTANDAO**

### TEKNOLOJIA JIKONI

Baada ya kusikia kuhusu uhaba na ughali wa kuni na mkaa uchunguzi ulifanywa kwenye baadhi ya maduka kuchunguza bei ya majiko ya kisasa yanayotumia nishati kwa ufanisi.

Jiko la presha (linalopika kwa mvuke) la umeme au 'electric pressure cooker' linaloelezwa kuwa hutumia umeme 'kiduchu' kupika vyakula vigumu kama kande na maharage, hupatikana kuanzia Shilingi 180,000.

Majiko hayo huuzwa kwenye maduka makubwa 'super market" na kwingineko lakini si rahisi kwa Watanzania wengi kuyamudu hasa wanaotumia kuni, vifuu, makumbi ya nazi.

Taasisi ya kuendeleza huduma za nishati endelevu TaTEDO, ni moja ya maeneo yanayozalisha jiko sanifu la umeme lenye presha (mvuke), ambalo linaelezwa hupika kwa ufanisi mkubwa na kwa nishati kidogo.

Ripoti za TaTEDO zinaeleza kuwa imefanya utafiti pamoja na vyuo vikuu vya kiteknolojia na kutengeneza jiko sanifu la umeme lenye mvuke (JULEP) linalopika kwa ufanisi mkubwa na kwa kutumia gharama ndogo ya umeme.

Baadhi ya vyakula vinavyopikwa ni makande ya kilo moja na nusu kwa dkakika 60 kwa umeme wa nusu 'unit' ikumbukwe 'unit' moja ya umeme ni shilingi 360 hivyo hutumia nusu au shilingi 180 kupika chakula hicho ambacho kwa mkaa kingepikwa kwa vipimo viwili vya Shilingi 3,000 kwa kuwa kipimo kidogo ni 1,500.

Aidha, maharage, nayo hutumia muda mfupi na unit chache za umeme jambo ambalo lingetunza mazingira kwa kupunguza moshi wa kuni angani unaoongeza hewa ukaa na kuokoa misitu.

Pengine ni wakati wa serikali kuanzisha mfuko wa nishati na kutoa ruzuku kwa wazalishaji wa majiko hayo kama TaTEDO ili kuwawezesha Watanzania wa kipato kidogo mijini na vijijini wasiomudu kupikia gesi na umeme kutumia majiko sanifu na kuokoa taifa na janga uhaba wa kuni na mkaa pamoja na misitu kutoweka.

Juhudi za kusambaza umeme vijijini ziende pamoja na kufikisha majiko sanifu ya umeme kwa wanavijiji ili walinde misitu.

## WANENAVYO MALENGA

## KUMBUKIZI YA MWALIMU

Huwezi kutenganisha, Nyerere na Tanzania,
Alifanya ya maisha, kabla ya Tanzania,
Tena lituimarisha, ile huru Tanzania,
Kumbukizi ya Mwalimu, hiyo ya vizazi vyote.

Mengi ya kufurahisha, yale alitufanyia,
Wakoloni kufurusha, mikono twamwinulia,
Hakusema yameisha, lizidi tutumikia,
Kumbukizi ya Mwalimu, hiyo ya vizazi vyote.

Falsafa lianzisha, bado tunazitumia,
Kwani nyingi za maisha, haziwezi kuishia,
Ari hizo zaamsha, Tanzania na dunia,
Kumbukizi ya Mwalimu, hiyo ya vizazi vyote.

Umoja liimarisha, Kiswahili kutumia,
Nchi aliunganisha, kote kimetufikia,
Hatuna jitambulisha, kikabila nakwambia,
Kumbukizi ya Mwalimu, hiyo ya vizazi vyote.

Utu alithaminisha, Tanzania na dunia,
Lifanya kuimarisha, hizi zetu jumuia,
Mataifa kuwezesha, uhuru kuufikia,
Kumbukizi ya Mwalimu, hiyo ya vizazi vyote.

Usawa litumezesha, sisi wote Tanzania,
Unyang'au likomesha, hakutaka kusikia,
Pazuri litufikisha, kweli tunafurahia,
Kumbukizi ya Mwalimu, hiyo ya vizazi vyote.

Mwalimu alifundisha, Ujamaa Tanzania,
Na pia ilimkosha, tujitegemee pia,
Hapo angetufikisha, tungetesa Tanzania,
Kumbukizi ya Mwalimu, hiyo ya vizazi vyote.

Nyenzo lizothaminisha, ndizo zinasaidia,
Amani kuidumisha, Afrika na dunia,
Wale tunu zawakosha, makwao wametulia,
Kumbukizi ya Mwalimu, hiyo ya vizazi vyote.

Wasomi watukumbusha, hapa tulipofikia,
Kama ngekuwa maisha, ngefika miaka mia,
Yalitoweka maisha, mema twayakumbukia,
Kumbukizi ya Mwalimu, hiyo ya vizazi vyote.

Kile kinafurahisha, vile wametuambia,
Njia hatujafupisha, hapa kwetu Tanzania,
Ya Mwalimu twafwatisha, amani twajivunia,
Kumbukizi ya Mwalimu, hiyo ya vizazi vyote.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

## FEDHA TARAKIMU

Fedha hizo tarakimu, na hazina mwisho hizo,
Kama wewe una hamu, kuzipata pesa hizo,
Kwa furaha ya kudumu, utakonda kwa mawazo,
Usikurubie pesa, hutaipata furaha.

Pesa tunaifahamu,kwa mambo mengi ni nguzo,
Ukiwa nazo ni tamu, kutatua matatizo,
Lakini ni tarakimu, bila mwisho ila mwanzo,
Usikurubie pesa, hutaipata furaha.

Hivyo wewe mwanadamu, ikae kwenye mawazo,
Furaha inayodumu, si zile pesa unazo?
Tengeneza tabasamu, kutaka pesa mzozo,
Usikurubie pesa, hutaipata furaha.

Furaha iliyo tamu, isokuwa na kikwazo,
Ulivyonavyo vitamu, si pesa ulizonazo,
Hazitoshi mwetu humu, tajiletea mzozo,
Usikurubie pesa, hutaipata furaha.

Kuridhika ni muhimu, hayo ya kwangu mawazo,
Ingawa pesa muhimu, sisake kimatangazo,
Jua hizo tarakimu, zimejaa maingizo,
Usikurubie pesa, hutaipata furaha.

Tarakimu zinadumu, ni sawa na hizi tozo,
Pesa nazo tarakimu, saka zisiwe tatizo,
Kitu kile ufahamu, hazitakupa tulizo,
Usikurubie pesa, hutaipata furaha.

Pesa jua tarakimu, kila zilipo ni mwanzo,
Hivyo usiweke hamu, zishike zile unazo,
Kutafuta ukidumu, utakuwa hamnazo,
Usikurubie pesa, hutaipata furaha.

Pesa hizo tarakimu, tarakimu zina mwanzo,
Mwisho hatuufahamu, wabakia kwenye wazo,
Tusijiweke ugumu, kusaka kwa nguvu hizo,
Usikurubie pesa, hutaipata furaha.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**





# PM aagiza mashauri yote ya watoto yatolewe uamuzi ndani ya miezi 6

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameviagiza vyombo vya sheria ikiwamo Jeshi la Polisi, Mahakama na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali (DPP), kufanyia kazi na kutoa uamuzi wa mashauri yote yanayohusu watoto ndani ya miezi sita na sio vinginevyo.

Pia, amezionya familia ambazo zimekuwa na tabia ya kumaliza kesi zinazohusu watoto zenyewe bila kufikisha mashauri katika vyombo vya sheria kuacha mara moja.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera na Uratibu wa Bunge, George Simbachawene, alibainisha hayo juzi alipokuwa akifungua kongamano la kitaifa la malezi ya watoto na familia kwa niaba ya Waziri Mkuu.

"Waziri Mkuu amenituma nitoe maagizo haya kwa vyombo vyote vya sheria nchini kuhakikisha kuwa mashauri yote yanayohusu watoto yanafanyiwa kazi na kutolewa maamuzi ndani ya miezi sita na sio vinginevyo," alisema Simbachawene.

Alisema hivi sasa matukio ya ukatili kwa watoto yamekuwa yakiongezeka na wahusika wakuu ni wanafamilia wenyewe.

Aidha, alisema jamii inapaswa kupaza sauti ili kupinga matukio ya ukatili kwa watoto kwa kuripoti katika vyombo vya sheria badala ya kumalizana kifamilia.

"Takwimu za Jeshi la Polisi zinaonyesha kuwa kuanzia Januari hadi Desemba, mwaka jana kesi za ukatili dhidi ya watoto zilizoripotiwa ni 11,499 ambapo matukio makubwa ni ubakaji 5,899, mimba 1,677 na ulawiti ni 1,114 na mengine mengi," alisema Simabachawene.

Kadhalika, alisema kutokana na hali hiyo vyombo vyote vya ulinzi vinapaswa kushughulikia kwa haraka na kutolea uamuzi mashauri yote yanayohusu mimba kwa watoto, ubakaji pamoja na ulawiti.

"Pia wazazi wote ambao watabainika kumaliza wenyewe kwa wenyewe mashauri yanayohusu ukatili dhidi ya watoto kama vile ubakaji, ulawiti na mimba wachukuliwe hatua kali za kisheria ili iwe fundisho kwa wengine," alisisitiza Simbachawene.

Vilevile, alisema moja ya sababu zinazochangia ongezeko la watoto wa mitaani ni migogoro katika familia inayosababisha ndoa kuvunjika na watoto kukosa malezi ya wazazi.

"Baadhi ya familia zinaishi bila upendo hali inayosababisha kutengana kwa wazazi na kusababisha ongezeko la watoto mitaani katika miji mbalimbali nchini, lakini serikali inaendelea kufanya jitihada za kumaliza hali hii ikiwamo ujenzi wa makao ya kulelea watoto nchini," alisema Simbachawene.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alisema serikali inatambua na inathamini familia kama chanzo cha nguvu kazi ya taifa.

"Hivyo katika kuimarisha uwezo wa familia kutimiza majukumu yake, serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, imekuwa ikitekeleza afua mbalimbali za kuwezesha familia kuishi kwa amani na upendo," alisema Dk. Gwajima.

Alisema baadhi ya afua hizo ni kutoa elimu ya malezi chanya kwa wataalamu wa halmashauri 7,445 wakiwamo maofisa Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii, Maofisa Lishe na walimu.

"Aidha, wataalamu hawa kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Juni 2021 walifanikiwa kutoa mafunzo na wazazi na walezi vinara (Champion) 110,805 ambao wamepewa jukumu la kuendeleza elimu ya malezi kwa wenzao katika mikoa 26 ya Tanzania Bara.

Alisema Tanzania inaungana na nchi nyingine duniani katika kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Familia inayofanyika kila mwaka Mei 15.

Maadhimisho ya mwaka huu yanafanyika kimkoa na mikoa yote 26 inafanya maadhimisho hayo kwa utaratibu ambao wanaona unafaa kulingana na mazingira yao.




Wawakilishi wa vituo vya watoa huduma ngazi ya jamii (CHWs) katika Shirika la Afya Shirikishi - Amref Tanzania, wakiwa katika mafunzo ya kutumia fursa zilizoko kwenye jamii kwa ajili ya kuzuia vitendo vya ukatili. Mafunzo hayo yalitolewa na Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Watumishi 437 wapandishwa vyeo Wizara ya Fedha

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ya Fedha na Mipango imewapandisha vyeo watumishi 437, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa hoja zilizoibuliwa na Baraza la Wafanyakazi, mwaka jana.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Jenifa Omolo, alibainisha hayo jijini hapo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kushiriki kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa wizara hiyo.

Omolo, alisema wizara hiyo imeshughulikia hoja zote zilizotolewa na watumishi katika Baraza la Wafanyakazi la mwaka jana kwa zaidi ya asilimia 90.

Alisema pamoja na kupandisha vyeo watumishi wake pia wizara hiyo imetoa Sh. bilioni 1.8 kwa ajili ya kuwapatia mikopo.

"Baraza lililopita watumishi waliwasilisha hoja mbalimbali ambazo walitaka zifanyiwe kazi ikiwamo, maslahi ya watumishi kupanda kwa mshahara, kupanda kwa vyeo, kuboresha mazingira ya kufanyia kazi ambayo kwa asilimia kubwa tumeshayafanyia kazi," alisema Omolo.

Aidha, alisema Baraza la Wafanyakazi ni chombo muhimu ambacho kinaiwezesha wizara kupata mawazo ya wafanyakazi ili kuyafanyia kazi.

"Katika baraza hili ambalo tumelifanya leo na jana watumishi pia wameibua hoja mbalimbali ambazo tunakwenda kuzifanyika kazi ili kuongeza tija katika utumishi wao, lakini suala la kupandishwa kwa mishahara hilo tayari kiongozi mkuu alishalitolea ufafanuzi hivyo tunaliacha kwa serikali.

"Hivi sasa tupo katika ujenzi wa jengo kule mji wa kiserikali Mtumba ili kupata ofisi ambayo itatosheleza mahitaji ya watumishi pia tunafanya ukarabati wa majengo ili kila mtumishi afanye kazi katika mazingira rafiki na kufanyia kazi changamoto ya uhaba wa watumishi katika maeneo mbalimbali," alisema Omolo.

Aliwasihi watumishi wa wizara hiyo kuendelea kufanya kazi na kuhudumia wananchi kwa ufanisi wakati serikali ikiendelea kuzifanyia kazi changamoto zote wanazao kabiliana nazo.

Pia alisema pamoja na mambo mengine ofisi yake imetoa mada za masuala ya afya na usalama mahala pa kazi pamoja na namna bora za kujilinda na magonjwa yasiyo ambukiza kwa watumishi ili kuwa na watumishi wenye afya bora.

Mhasibu Mkuu wa Serikali, Leonard Mkude, aliwataka wastaafu wote nchini kuwa makini na wimbi la matapeli ambalo limeibuka kutafuta taarifa zao na kuahidi kuwasaidia kwa kuwatoza fedha.

"Huduma zetu zote ni bure kama mstaafu anashida atoe taarifa katika ofisi zetu za hazina badala ya kuwasikiliza matapeli ambao wamekuwa wakidai wawapatie kiasi cha fedha ili waweze kuwasaidia katika kulipwa stahiki zao," alisema Mkude.

## STAMICO, ABSA zasaini makubaliano uchimbaji wa makaa ya mawe

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SHIRIKA la Madini la Taifa (STAMICO) na Kampuni ya ABSA ya Uswiss, zimesaini mkataba wa makubaliano ya uchimbaji wa makaa ya mawe mkoani Songwe katika Mgodi wa Kabulo na tani 60,000 zitauzwa kwa mwezi kwa wawekezaji hao kwa kipindi cha miaka mitano.

Hafla ya utiaji saini mkataba huo kati ya STAMICO na mwekezaji Kampuni ya ABSA ya nchini Uswiss umefanyika juzi jijini Dodoma na kushuhudiwa na Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa.

Akizungumza katika hafla hiyo, Dk. Kiruswa, alisema kutokana na mradi huo STAMICO itakusanya mapato ya wastani wa Sh. bilioni 4.16 kwa mwezi sawa na wastani wa Sh. bilioni 50 kwa mwaka.

Alisema, STAMICO itatoa ajira 600 na fursa nyingine za ajira kwa Watanzania katika mradi huo na kusaidia kukuza uchumi wa mwananchi mmoja mmoja hali itakayo punguza umaskini.

Kadhalika alimpongeza Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa STAMICO, Dk. Venance Mwasse na Menejimenti yake kwa kuwa wabunifu katika kutafuta masoko nje ya nchi.

"Naishukuru STAMICO kwa maamuzi ya kukubaliana na Kampuni ya ABSA katika kufanya biashara hapa nchini matumaini yangu kuwa makubaliano haya yaliyosainiwa yatakuwa na manufaa kwa pande zote mbili," alisema Dk. Kiruswa.

Akizungumzia mafanikio ya STAMICO, Dk. Kiruswa alisema, katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Machi 2022, katika mradi wa Kabulo, tani 17,324 za makaa ya mawe zilichimbwa na 12,792 zenye thamani ya Sh. bilioni 1.2 ziliuzwa na kulipa serikalini Sh. 174,191,290.87 ikiwa ni mrabaha na ada ya ukaguzi.

Dk. Kiruswa alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuifungua nchi kibiashara ili wawekezaji kuja kuwekeza nchini.

"Tanzania ni nchi salama kwa uwekezaji, niwahakikishie wawekezaji wetu wa makaa ya mawe kuwa usalama uliopo utazingatia pia ulinzi wa wawekezaji na mali zao, nchi yetu inajali wawekezaji na kuzingatia sheria za kimataifa hivyo wizara hii itahakikisha inafuatilia mwenendo mzima wa mkataba huu ili kupata matokeo chanya kwa Shirika na Kampuni ya ABSA," alisema.

Naye Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa STAMICO, Dk. Venance Mwasse, alisema tukio hilo ni matokeo ya mkakati wa kuanza uchimbaji mkubwa wa makaa ya mawe.

Pia alieleza kuwa maandalizi yamekamilika katika ukarabati wa miundombinu ya barabara, daraja na mgodi wa chini na uchimbaji umeanza.

Dk. Mwasse alisema, STAMICO imesaini mkataba mkubwa wa kihistoria na itauza tani 60,000 kwa mwezi za makaa ya mawe.



# Waandishi wasio na mikataba wahofu nyongeza mishahara

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

LICHA ya Rais wa Tanzania Samia Suluhu Hassan kutangaza nyongeza ya mshahara kwa asilimia 23.3 kwa watumishi mbalimbali nchini, nyongeza hiyo inaweza isiwanufaisha baadhi ya waandishi nchini ambao hawana mikataba ya ajira licha ya kufanya kazi kubwa ya kuihabarisha jamii. Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili na Mafunzo kutoka Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari nchini (UTPC), Frank Leonard, alisema hayo jana alipozungumza na wanahabari wa mkoa huo wakati wa maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari, kuwa nyongeza hiyo ya mshahara ni maumivu kwa wanahabari ambao hawana ajira wala mikataba.

Alisema kutokana na hali hiyo ni wakati wa wanahabari nchini kushikamana kuwahamasisha wamiliki wa vyombo vya habari kutoa mikataba na ajira kwa watumishi wao ili kupata fedha za kujikimu na kuendesha maisha yao.

"Nyongeza ya mshahara imekuwa ni neema kwa waajiriwa na wenye mikataba, lakini sisi baadhi yetu wanahabari tusio na ajira wala mikataba ni maumivu, tunaiomba serikali iangalie namna ya kuwabana wamiliki wa vyombo vya habari kutoa ajira wa wanahabari nao wafurahie nyongeza hiyo na kumudu gharama za maisha," alisema Leonard.

"Tunafanya kazi kama kuku wa kienyeji licha ya jukumu kubwa tulilonalo ya kupaza sauti kwa wasiokuwa na sauti lakini wakati mwingine kutokana na ugumu wa maisha tunalazimika kuingia kwenye mitego na kushindwa kusimamia misingi yetu," aliongeza Leonard.

Mgeni rasmi katika maadhimisho hayo, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alikiri kuwapo kwa tatizo kubwa la ajira na mikataba kwa wamiliki wa vyombo vya moto.

Kutokana na tatizo hilo, Dk. Chuachua aliahidi kukutana na wamiliki wa vyombo vya habari wa Jiji la Mbeya kufanya kikao cha pamoja na kuja na maazimio ya kuboresho maslahi ya wanahabari.

Pia, aliviomba vyombo vyote vya habari nchini kujali na kuthamini mchango wa watumishi wao kwa kuhakikisha wanawapatia mikataba na ajira ili kuendesha maisha yao kama watumishi wengine hapa nchini.

Aliwapongeza wanahabari kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhabarisha wananchi masuala mbalimbali yanayofanyika nchini na kuwaomba kuendelea kuwa wazalendo na kuandika masuala yanayoitangaza vyema Tanzania.

Katika maadhimisho hayo ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani yenye kauli mbiu isemayo, "Waandishi wa Habari na changamoto za kidigitali," kwa Mkoa wa Mbeya yalifanyika jana pamoja na uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mbeya Press Club.

Katika uchaguzi huo kulikuwa na wajumbe 31 waliopiga kura kati ya 52, kura 21 zilimpatia ushindi Nebart Msokwa.

Baada ya uchaguzi huo, msimamizi wa uchaguzi, Felix Mwakyembe, alimtangaza Nebart Msokwa ambaye ni mwanahabari wa Gazeti la Nipashe kuwa Mwenyekiti mpya wa Mbeya Press Club baada ya aliyekuwa Mwenyekiti wa MBPC, kufariki dunia mwanzoni mwa mwaka huu.



Mwenyekiti mpya wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Mbeya, Nebart Msokwa (katikakti) ambaye ni mwandishi wa habari katika gazeti la Nipashe, akiandika baadhi za hoja za wajumbe baada ya kutangazwa kuwa mshindi wa nafasi hiyo jana. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua aliyekuwa mgeni rasmi na kushoto ni Makamu Mwenyekiti wa Klabu hiyo, Joseph Mwaisango. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Waomba utaratibu wa fidia wauguzi wapatapo maambukizi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAUGUZI mkoani hapo wameiomba serikali kuandaa utaratibu wa kuwalipa fidia wahudumu wa afya wanaopata athari wakiwa kazini, ikiwa ni pamoja na kupata maambukizi ya magonjwa ya mlipuko wakati wa kuwahudumia wagonjwa hao.

Wauguzi hao walitoa ombi hilo wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wauguzi Duniani ambayo kimkoa yalifanyika wilayani Mbarali.

Mwenyekiti wa Chama cha Wauguzi Mkoa wa Mbeya, Abel Nyalusi, alisema miongoni mwa vikwazo wanavyokabiliana navyo wakati wa kutekeleza majukumu yao ni hatari ya kupata maambukizi kutoka kwa wagonjwa wanapohudumia.

"Siku hii muhimu kwetu sisi wauguzi inatupa nafasi ya kutathmini utendaji kazi wetu sambamba na serikali kutambua vikwazo vinavyotukabili ikiwamo uhaba wa vifaa tiba, miundombinu mibovu hususani majengo kwa ajili ya kutolea huduma za matibabu sana maeneo ya vijijini," alisema Nyalusi.

Aliiomba serikali kuendelea kuboresha miundombinu ya majengo kama vifaa, nyumba za walimu na wagonjwa ili kutoa huduma za matibabu kwa wakati na kuokoa uhai wa wananchi.

Kwa upande wake, Katibu wa Chama cha Wauguzi Mkoa wa Mbeya, Jacob Kashililika, alimpongeza Mkuu wa Mkoa wa Mbeya kwa kuendelea kuwaunganisha pamoja wataalamu wa afya na kutatua vikwazo vinavyowakabili.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Dk. Godfrey Mwakalila, alisema kuwa miongoni mwa mambo anayojivunia katika wilaya yake ni wauguzi kuungana kuwa kitu kimoja na kutekeleza majukumu yao kwa moyo mmoja.

Aliwaomba wataalamu wenzake wa afya kuendelea kutoa huduma bora za matibabu kwa kuhakikisha wanazingatia maadili na misingi ya utoaji wa huduma za afya.

# Vikundi vyaahidiwa neema uzalishaji mboga, matunda

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

VIKUNDI vya wanawake na vijana vilivyofanya vizuri kwenye utekelezaji wa Mradi wa Feed The Future Tanzania mboga na matunda, vimeahidiwa kuimarishwa zaidi ili viendelee kutoa mchango kwenye mapambano dhidi ya udumavu na utapiamlo katika mikoa ya Mbeya na Songwe.

Miongoni mwa matokeo chanya yaliyobainika katika utekelezaji wa mradi huo ulioendeshwa kwa miaka mitano na nusu nchini katika mikoa mbalimbali ikiwamo Mbeya na Songwe kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Msaada la Watu wa Marekani (USAID) ni pamoja na uzalishaji wa mazao lishe yanayotumika kwa milo ya wajawazito na watoto walio na umri wa chini ya miaka mitano.

Meneja wa mafunzo, ufuatiliaji na uthamini wa mradi huo, Stephen Mruma, alibainisha hayo juzi katika kikao kazi cha kutoa tathmini ya mradi huo ulioanza kutekelezwa nchini tangu Januari 2017 kilichowakutanisha wadau kutoka halmashauri za mikoa ya Mbeya na Songwe kikifanyika jijini hapa.

Mruma alisema kwa vikundi vingi vya vijana kujihusisha na kilimo cha mboga na matunda kupitia mradi huo kuliwezesha jamii kuvipata kwa urahisi vyakula muhimu vinavyohitajika kwa ajili ya lishe bora za wajawazito, mama wanaonyonyesha na pia watoto hasa iliposhauriwa na wataalamu wa afya.

Wadau waliohudhuria kikao kazi hicho walisema kuna kila sababu ya vikundi vilivyofanya vizuri kwenye mradi huo kupewa msukumo zaidi wa kuendeleza uzalishaji ili kuvipa uwezo zaidi wa kuchangia kuiondoa mikoa hiyo kwenye wastani wa asilimia 43 ya udumavu unaotajwa kuwapo.

Miongoni mwa wadau walioahidi kuwa wa kwanza kuyapa uwezo makundi hayo ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Missana Kwangura, alisema kwa kuwa mradi umekuja na majibu ya kutatua tatizo la udumavu, vikundi husika vitaingizwa kwenye mpango wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu ambayo hutolewa kila mwaka wa fedha kutoka mapato ya ndani.

"Kumekuwa na tatizo kubwa la udumavu na utapiamlo licha ya mikoa yetu kuongoza katika uzalishaji wa mazao mbalimbali yakiwamo ya chakula. Yote haya yamekuja kupatiwa majibu kutokana na mradi. Lazima mradi uendelezwe na vikundi vya wanawake na vijana vilivyoshirikishwa tutaviwezesha ili uzalishaji wa mazao lishe uendelezwe," alisema Kwangura.

Meneja miradi wa Shirika la Kilimo la wilayani Ileje mkoani Songwe (IRDO), Patrick Mwalukisa, alikitaja kijiji cha Ivuna kilichoko wilayani Momba kuwa miongoni mwa maeneo yaliyokuwa na ugumu kwa kilimo cha mbogamboga na matunda kutokana na uwepo wa wafugaji korofi licha ya kuwa na mazingira rafiki ya kilimo cha bustani.

Mwalukisa alisema baada ya ujio wa Mradi wa Feed The Future Tanzania, Mboga na Matunda, wakazi wa kijiji hicho na maeneo ya jirani wameondokana na adha ya kufuata umbali mrefu hadi mji wa Mlowo, kufuata mbogamboga na matunda na kuendesha kilimo na kudhibiti mifugo na hivyo kuwezesha jamii kupata milo bora iliyo na lishe sahihi ikiweo inayohitajikwa kwa wajawazito, wanaonyonyesha na watoto wadogo.

Alishauri serikali na wadau katika maeneo mengine, kuiga mfano wa kijiji hicho namna ulivyotumia utekelezaji wa mradi husika kubadili mwenendo wa wafugaji na kutoa mwanya kwa vijana na wanawake, kuendesha shughuli za kilimo cha mazao ya matunda na mbogamboga na kuanza kukiondoa kijiji kwenye mzazingira ya lishe duni, udumavu na utapiamlo.

Ofisa Kilimo Wilaya ya Momba, Oscar Mwilongo, aliitaja kata ya Msangano wilayani hapo kuwa miongoni mwa maeneo ambayo jamii inakabiliwa na dalili za utapiamlo na udumavu kutokana na kukosa lishe bora kwa sababu ya ufinyu wa upatikanaji wa baadhi ya vyakula, ikiwamo mboga na matunda hatua aliyosema inasababishwa na ufugaji holela unaokwamisha kilimo cha bustani.

Akifunga kikao kazi hicho, Katibu Tawala msaidizi Mkoa wa Songwe anayesimamia Uchumi na Uzalishaji, Vansca Kulanga, aliwasihi vijana na wanawake walioshiriki utekelezaji wa mradi huo kuunda vikundi ili wanufaike na mikopo kutoka kwenye halmashauri zao na kuendelea na uzalishaji.



# Vituo 10 vya polisi vyafungwa changamoto uendeshaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALi ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema jumla ya vituo vidogo 10 vya polisi vimefungwa kwa sababu mbalimbali ikiwamo changamoto za uendeshaji pamoja na kuimarika kwa ulinzi kwa jamii.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Hamza Hassan Juma, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini, Machano Othman Said katika kikao cha baraza hilo, aliyetaka kujua kwa nini vituo vidogo vingi vya Jeshi la Polisi vimefungwa wakati matukio ya uhalifu yakiendelea.

Juma alikiri baadhi ya vituo kufungwa Unguja na Pemba kutokana na changamoto za kiuendeshaji ambazo zilikuwa zikilikabili Jeshi la Polisi.

Alizitaja changamoto hizo ni pamoja na uhaba wa askari katika kuviendesha na kuvisimamia vituo hivyo na gharama za uendeshaji.

Alisema kuimarika kwa polisi jamii kwa kiasi kikubwa kumesaidia kupunguza kuwapo kwa vituo vya polisi kwa sababu wananchi wenyewe wamehamasika na ulinzi shirikishi kupambana na matukio ya uhalifu.

"Mheshimiwa Spika serikali imehamasisha ulinzi shirikishi ambao lengo lake kubwa kusimamia masuala ya ulinzi katika jamii hatua ambayo imepunguza uhalifu," alisema.

Juma alisema Jeshi la Polisi lipo tayari kupokea maombi ya ujenzi wa vituo vya polisi kulingana na mahitaji ya wananchi.

Alisema hayo wakati akifafanua swali la Mwakilishi wa Jimbo la Kojani Pemba, Omaar Hassan, aliyetaka kujua lini Kituo cha Polisi cha Ole Kengeja na Ole Kianga, kitajengwa ili kukabiliana na matukio ya uhalifu ikiwamo usafirishaji wa mazao ya chakula.

"Jeshi la Polisi lipo tayari kupokea maombi ya wananchi wanaotaka kujengwa kwa vituo vya polisi kulingana na mahitaji yao katika kukabiliana na uhalifu na kuweka usalama wa raia," alisema.

# Kampuni sasa kusimamia kilimo cha mwani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imetangaza rasmi kuundwa kwa kampuni itakayosimamia maendeleo ya kilimo cha mwani ambacho kwa asilimia 85 kinalimwa na wanawake.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022-2023 katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Shaaban alizitaja sababu zilizoifanya SMZ kuunda kampuni ya mwani ni kusimamia maendeleo ya kilimo hicho pamoja na kukabiliana na changamoto zilizopo kuona kilimo hicho kinakuwa mkombozi kwa wakulima visiwani humo.

Alisema malengo mengine ya kuanzishwa kwa kampuni hiyo ni kutafuta masoko mapya ya kilimo hicho kwa ajili ya kuongeza kipato kwa wakulima.

Alisema kwa muda mrefu kilimo cha mwani kimekuwa kikishughulikiwa moja kwa moja na wafanyabiashara binafsi na kuibua malalamiko makubwa kwa wakulima wenyewe ikiwamo kuyumba kwa bei kutoka kwa wakulima kiasi ya kukata tamaa.

"Hizo ndiyo sababu kubwa zilizopelekea Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuunda kampuni itakayosimamia moja kwa moja maendeleo ya kilimo cha mwani visiwani," alisema.

Alizitaja sababu zingine zitakazofanywa na Kampuni ya Mwani ni kufanya utafiti kuhusu maendeleo ya kilimo hicho ambacho kinakabiliwa na changamoto kubwa ikiwamo mabadiliko ya tabia ya nchi na kukumbwa na maradhi mbalimbali.

"Changamoto kubwa zinazokikabili kilimo cha mwani kwa sasa ni kuibuka kwa maradhi mbalimbali ambayo yamekuwa yakisababishwa na mabadiliko ya tabia ya nchi na kilimo hicho kuyumba uzalishaji wake na kuwakatisha tamaa wakulima wake," alisema.

Waziri Shaaban alisema serikali ipo katika hatua za mwisho mradi wa ujenzi wa kiwanda cha kusarifu na kuongeza thamani ya zao hilo ambacho kinatarajiwa kujengwa Chamanangwe Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Alisema serikali imetenga Sh. milioni 444 kwa ajili ya kampuni ya mwani ambayo itanunua mwani jumla ya tani 1,200.

Alisema kampuni hiyo inatarajiwa kuingiza fedha jumla Sh. bilioni 2.031 zinazotokana na mauzo ya kilimo hicho nje ya nchi.

"Mheshimiwa Spika napenda niwajulishe wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba wizara inakusudia kujenga kiwanda cha kusarifu na kuongeza thamani ya kilimo hicho ambacho kitahusisha sekta binafsi huko Chamanagwe Pemba," alisema.




Mwakilishi wa Jimbo la Malindi, Muhamed Ahmada, akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wawakilishi wataka kijengwe kiwanda kusindika ndimu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wameitaka Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kujenga viwanda vidogo vya kusindika mazao ya kilimo ikiwamo ndimu kwa ajili ya kuongeza thamani na wakulima kupata tija.

Akichangia bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022-2023, Mwakilishi wa Jimbo la Chwaka, Issa Haji Ussi, alisema wakulima wameitikia wito wa kilimo cha uzalishaji wa ndimu, lakini hadi sasa wanakabiliwa na kukosa kiwanda kitakachosindika zao hilo na kuongeza thamani yake.

Alisema kitendo cha kukosa kiwanda cha aina hiyo kwa kiasi kikubwa kimewavunja moyo wakulima wa kilimo hicho wanaozalisha ndimu nyingi ambazo matokeo yake huoza.

"Mheshimiwa Spika kilio kikubwa cha wakulima wa kilimo cha ndimu katika Jimbo la Chwaka wanahitaji kiwanda kitakachoongeza thamani ya matumizi ya ziada ya zao hilo kwa ajili ya kuwaingizia kipato...hadi sasa hakuna kiwanda cha kuhifadhi uzalishaji wa ndimu," alisema.

Mwakilishi wa Jimbo la Ziwani, Suleiman Makame, aliitaka Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, kujikita zaidi katika utekelezaji wa miradi ya viwanda vidogo vidogo ambavyo ndiyo mkombozi kwa wakulima na wazalishaji wengine wa bidhaa mbalimbali za kilimo.

Alisema wakulima wa mazao ya embe na ndimu wanahitaji viwanda vya aina hiyo vitakavyosindika mazao yao kwa ajili ya kupata kipato kikubwa katika soko.

Alisema kisiwa cha Pemba kinaongoza kwa uzalishaji wa embe za aina mbalimbali na mahitaji ya viwanda vidogo vidogo vya kusindika na kuongeza thamani vinahitajika kwa sasa ili kuwakomboa wakulima.

"Mheshimiwa Spika wakulima wetu kilio chao kikubwa wanahitaji viwanda vidogo vidogo vitakavyosindika mazao yao na kuongeza thamani ya uzalishaji na kuingia katika soko na kupata kipato kikubwa," alisema.

Mwakilishi wa Viti Maalumu, Mkoa wa Kaskazini Pemba, Bihindi Hamad, alisema wakulima wa Jimbo la Micheweni wamehamasika uzalishaji wa mazao mbalimbali ambayo wanahitaji viwanda vitakavyoongeza thamani na ubora wa bidhaa zao kuingia sokoni.

"Wakulima wetu wanazalisha nyanya nyingi, lakini hatuna soko na kiwanda cha kusindika na kuongeza thamani na matokeo yake zinaharibika katika kipindi kifupi na kuwakatisha tamaa wakulima watu," alisema.

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeyatenga maeneo ya Chamanangwe pamoja Dunga na Donge kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya viwanda vya aina mbalimbali nchini.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya mwanzo ya wilaya ya Njombe**

**Kituo cha Njombe mjini**
**Mkoa Njombe**

**Usimamiziwa mrathi Na 37/ 2022**

**Katika shauri la mirathi ya MWAJABU SEKALINGA.....Marehemu Wa KWIVAHA**

**Katika shauri la maombi ya kumteua msimamizi yaliyoletwa na KENANY MBEYELA......Mwombaji.**

**TANGAZO KWA UMMA.**

**(Kanuniya 5(2) yakanuni za usimamizi wa Mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja kuudhuria katika shauri hili endapo wakita kakufanya hivyo mnamo tarehe ...11.......mwezi ...06..... mwaka... 2022..... kabla ya huyo muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo ,mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa kabla au mpakata rehetajwa hapo juu.

**Zingatia;**Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

* Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

**Imetolewa leo tarehe...11.... mwezi ...05.... Mwaka...2022.....**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MARY C MKOLO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1495-0026** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia **GENESIS HIGH SCHOOL** mwaka 2014,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi, Polisi taarifa **MKB/RB/962/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**WILLIAM JOHN MTALUHA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **MAZDA DEMIO** yenye usajili namba **T 462 DUT,** CHASSIS NAMBA: **DY3W233761,** ENGINE NAMBA: **ZJ277955.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

TAARIFA POLISI:
**MKB/TR/RB/94/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ELIZABETH ELIRINGIA MLAY** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato che nne chenye index namba S.4024/0038 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **USAMBARA GIRLS SEKONDARI** mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi:**
**DSM/PHQ/RB/190959/2022.**

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Wabunge Somalia wamchagua rais

**MOGADISHU,** SOMALI

MOHAMUD alimshinda Mohammed Abdullahi Farmajo ambaye alipata kura 110, wakati kura tatu ziliharibika.

Mohammed Abdullahi farmajo aliingia madarakani mwaka 2017, lakini alijikuta akianguka kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ucheleweshwaji wa uchaguzi.

Kwa matokeo hayo yanamrudisha madarakani kwa mara ya pili Hassan Sheikh Mohamud, ambaye alitawala kati ya 2012 hadi 2017.

Uchaguzi huo ambao ulikuwa na ushindani mkali na uliingia katika raundi ya tatu, ulicheleweshwa kwa miezi 15 kutokana na vita na masuala ya usalama.

Mohamud aliapishwa muda mfupi baada ya matokeo ya mwisho kutangazwa, na kuwafanya wafuasi wake katika mji huo kumpongeza na kufyatua risasi hewani.

Katika uchaguzi huo wa Jumapili, mamia ya wabunge walipiga kura zao katika anga moja la ndege katika mji mkuu wa Mogadishu.

Milipuko ilisikika karibu na eneo hilo huku uchaguzi ukiendelea lakini maofisa wa polisi walisema kwamba hakuna mtu aliyejeruhiwa. **BBC**



# Vita vyapamba moto Ukraine, kila upande wadai kushinda

**KYIV,** UKRAINE

WANAJESHI wa Ukraine wanaolinda mji wa kaskazini wa Kharkiv, inadaiwa wamefika kwenye mpaka kati ya nchi hiyo na Russia.

Gavana wa mji huo, Oleh Sinegubov alitoa madai hayo katika ujumbe wake alioutuma kupitia mtandao wa Telegram.

Hata hivyo, bado madai hayo hayajathibitishwa na haijafahamika mara moja ni wanajeshi wangapi walikuwa wamefika kwenye mpaka wa Russia na ni wapi.

Wizara ya ulinzi ya Ukraine imechapisha video inayodaiwa kuwaonyesha wanajeshi kadhaa kutoka kikosi cha ulinzi wa eneo wakiwa katika sehemu hiyo isiyojulikana kwenye mpaka.

"Tumefika, tuko hapa," mmoja wa askari alisema. Ukraine imekuwa ikipambana na kuwarudisha nyuma wanajeshi wa Russia kutoka Kharkiv, mji wa pili kwa ukubwa nchini Ukraine.

### SWEDEN YAAPA KUJIUNGA NATO

Sweden imethibitisha kuwa itawasilisha maombi ya kujiunga uanachama wa Nato katika mabadiliko ya kihistoria kutokana na uvamizi wa Russia dhidi ya Ukraine.

Jana Waziri Mkuu wa Sweden, Magdalena Andersson, anatarajiwa kwenda bungeni kupata uungaji mkono kwa ajili ya maombi hayo, na pia ataongoza kikao maalum cha baraza la mawaziri kuzungumzia suala hilo.

Hatua hiyo inakuja baada ya chama chake cha Social Democratic, kuacha upinzani wake wa muda mrefu wa kujiunga na muungano wa Nato.

Awali, Andersson alisema msimamo wa kutofungamana na upande wowote kwa jeshi lake kuliisaidia Sweden miaka iliyopita, lakini kwa sasa huenda isifanye hivyo.

### BELARUS KUTUMA VIKOSI

Belarus imetangaza kupeleka vikosi maalum vya operesheni kwenye mpaka wa Ukraine, Wizara ya Ulinzi ya Uingereza ilisema katika taarifa zake za kijasusi.

Taarifa hiyo ilisema pia imetuma vitengo vya ulinzi wa angani, silaha na makombora kwa mazoezi ya kijeshi magharibi mwa nchi hiyo.

Uwepo wa vikosi vya Belarus karibu na mpaka wa Ukraine kunaweza kuwazuia wanajeshi wa Ukraine ili kutoweza kupeleka wanajeshi zaidi kusaidia katika operesheni za jimbo la Donbas, lakini inaongezea kwamba kufikia sasa vikosi vya Belarusi havijahusika moja kwa moja katika mzozo huo.

### NATO KUANZA MAZOEZI YA KIHISTORIA

Mazoezi makubwa ya kijeshi kwa nchi za muungano wa kujiami ya Nato, yalianza jana.

Taarifa zilisema mazoezi hayo yanafanyika katika taifa la Estonia kwa kipindi cha wiki mbili yanawahusisha wanajeshi 15,000 kutoka nchi kumi, zikiwamo Uingereza, Marekani na wajumbe wa nchi za Finland na Sweden.

Licha ya kwamba mazoezi hayo yalikuwa yamepangwa hata kabla ya Russia kuanza uvamizi wake nchini Ukraine, yameibua kwa kiasi kikubwa wasi wasi baina ya Nato na Russia.

Mazoezi hayo yameelezewa kuwa ni muhimu kwa mataifa ya Baltic, kwani lengo lake ni kufanya majaribio ya uwezo wao katika kujibu uvamizi sawa wa maadui.

### MAZUNGUMZO YAANZA MARIUPO

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, alisema kuwa wanafanya juhudi kubwa kuhakikisha wanawaondosha wanajeshi wao waliojeruhiwa katika jimbo la Mariupol.

Zelensky alitoa kauli hiyo katika matangazo ya kila wiki ambayo amekuwa akiyatoa tangu uanze uvamizi wa Russia dhidi ya nchi yake.

Jeshi limetoa wito wa msaada baada ya wanajeshi wengi kujeruhiwa.

Hapakuwa na njia ambayo wangeweza kuitumia kutoroka kwasababu jeshi la Russia lilikuwa limezingira eneo hilo.

Katika hotuba hiyo, Rais Zelensky, alisema kuwa wameanza mazungumzo ya kuangalia iwapo vikosi vya Russia vitaruhusu kuwaondoa majeruhi.

Lakini Zelensky pia alisema yalikuwa ni mazungumzo magumu mno.

Hakuwataja wawakilishi wa Ukraine katika mazungumzo hayo, lakini alisema ni wao waliotaka yaanzishwe. **BBC**



Muuguzi akimsafisha majeraha mwanajeshi wa Ukraine, Maksim, ambaye amejeruhiwa katika mapambano yanayoendelea na Russia hivi karibuni. **PICHA: REUTERS**

# Raila Odinga amteua Martha Karua makamu rais

**NAIROBI,** KENYA

WAZIRI Mkuu wa zamani wa Kenya, Raila Odinga, amemteua Martha Karua kuwa mgombea mwenza wake, na kumfanya kuwa mwanamke wa kwanza kuwania nafasi hiyo nchini humo.

Wakati akitaja jina lake, Odinga alisema Ofisi ya Naibu wa Rais haiwezi kushindana na urais, na anayeshikilia wadhifa huo lazima awe mfanyakazi mwenza.

Karua, alijiunga na muungano wa Azimio mwezi Machi, amekuwa akizunguka nchi nzima akipigia debe uungwaji mkono kwa Odinga.

Iwapo atachaguliwa mwezi Agosti, mwanasiasa huyo mkongwe atakuwa naibu wa rais wa kwanza mwanamke wa Kenya.

Chaguo la Martha Karua limeleta mgawanyiko ndani ya muungano huo na kusababisha kiongozi wa Chama cha Wiper Kenya na makamu wa rais wa zamani Kalonzo Musyoka, ambaye alikuwa akipigiwa upatu kutangaza kujitenga na muungano huo.

Katika kikao tofauti na wanahabari, Musyoka alimtakia Karua kila la heri.

"Namtakia kheri mgombea mwenza Martha Karua. Tumekubali kwenda njia tofauti. Nilimwambia Raila uamuzi wa kuchagua Karua utakabiliwa na upinzani mkubwa. OKA itapambana kivyake na hivi karibuni Wiper itazindua ilani yake yenyewe," alisema. **BBC**

# WASHINDANI WA SIMBA KUVAANA FAINALI CAF

**Na Adam Fungamwango**

TIMU mbili zilizocheza dhidi ya Simba kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika (CAF), RS Berkane ya Morocco na Orlando Pirates ya Afrika Kusini, zimetinga fainali ya michuano hiyo, baada ya kufanya vizuri kwenye mechi zao za nusu fainali.

RS Berkane ambayo ilikuwa Kundi D pamoja na wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano hiyo, Simba, juzi ilifanikiwa kutinga fainali kwa kuichakaza TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo mabao 4-1 kwenye Uwanja wa Manispaa wa Berkane yakiwekwa wavuni na Bark El Helali, Larbi Naji na Youssef El Fahli akifunga mawili, moja kwa mkwaju wa penalti, huku la kufutia machozi la TP Mazembe likifungwa na Phillipes Kinzumbi.

Timu hiyo inatinga fainali kwa jumla ya mabao 4-2, kutokana na kufungwa bao 1-0 ugenini nchini DR Congo zilipokutana Mei 8, mwaka huu.

Kwenye hatua ya makundi, Simba ilicheza dhidi ya RS Berkane kwenye mechi ya kwanza ugenini nchini Morocco Februari 27, na kuchapwa mabao 2-0, lakini mechi ya marudiano iliyochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Machi 13, mwaka huu ilishinda bao 1-0 lililowekwa wavuni na Pape Sakho.

Timu nyingine iliyotinga fainali ni Orlando Pirates licha ya kipigo cha bao 1-0 nyumbani Uwanja wa Orlando ulioko kitongoji cha Soweto, dhidi ya Al Ahli Tripoli ya Libya, Wasauzi hao wamesonga mbele kutokana na ushindi wa mabao 2-0 walioupata Mei 8, mwaka huu, wakiwa ugenini.

Bao la Ali Abu Arqoub, halikutosha kuyapiku yale ya Innocent Maela na Goodson Mosele yaliyofungwa nchini Libya na kuifanya Orlando kutinga fainali kwa jumla ya mabao 2-1.

Wasauzi hao walitinga hatua hiyo kwa kuitoa Simba kwa mikwaju ya penalti 4-3, Aprili 24 nchini humo baada ya kila timu kushinda bao 1-0 nyumbani.

Aprili 17, mwaka huu Simba ilishinda bao 1-0 la Shomari Kapombe kwa mkwaju wa penalti, baada ya kupoteza kwa bao 1-0 ugenini, na kisha changamoto ya mikwaju ya penalti kuchukua nafasi yake na kisha Orlando kunufaika nazo.

**KOMBORA...**



Kiungo mshambuliaji wa Yanga, Dickson Ambundo, akiudhibiti mpira kabla ya kuachia kombora kali lililomshinda kipa Mohamed Yusuph, na kujaa wavuni moja kwa moja, hivyo kuiandikia timu yake bao la kwanza wakati ikishinda 2-0 dhidi ya Dodoma Jiji kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma juzi. **PICHA: YANGA**

# *Ihefu yaapa kutorudia makosa Ligi Kuu*

**Na Saada Akida**

BAADA ya kukata tiketi rasmi ya kurejea tena Ligi Kuu msimu ujao, uongozi wa Klabu ya Ihefu, umesema hautakubali kufanya makosa waliyofanya msimu uliopita na kusababisha kushuka daraja na kucheza Ligi ya Championship msimu huu.

Klabu ya Ihefu imekuwa timu ya pili kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya DTB FC, ambayo iko kileleni mwa msimamo wa Ligi ya Championship inayoelekea ukingoni.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa klabu hiyo, Juma Nyauba, alisema wamejiandaa vizuri kwa ajili ya msimu ujao na wanatarajia baada ya kumalizika kwa mchezo wao wa mwisho dhidi ya Ndanda FC, watapokea ripoti kutoka kwa Kocha wao, Zuberi Katwila.

Alisema wanatambua msimu uliopita walishuka daraja kutokana na makosa waliyofanya na sasa hawataki kurejea tena huko, hivyo watahakikisha wanafanya usajili wa uhakika kulingana na mapendekezo ya benchi lao la ufundi.

"Ni jambo la furaha kurejea katika Ligi Kuu msimu ujao, lakini tumejifunza kutokana na makosa ya msimu uliopita, tutahakikisha tunafanya usajili mzuri ili kuimarisha timu yetu," Nyauba alisema.

"Hatutaki kuingia katika siasa ambazo zilitufanya tukacheza msimu mmoja katika ligi, hilo jambo hatutaki lijirudie, tunataka kuhakikisha tunaenda kuleta ushindani mkubwa kwenye Ligi Kuu."

## Zimamoto yataka nafasi ya pili Z'bar

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

MALENGO makuu ya timu ya Maafande wa Zimamoto sasa ni kumaliza nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu Zanzibar baada ya uwezekano wa kutwaa ubingwa wa ligi hiyo kutoweka, imeelezwa.

Mafande wa Zimamoto hao, wapo nafasi ya sita katika msimamo wa ligi hiyo wakiwa na alama 44 huku timu inayoshika nafasi ya pili kwa sasa, Maafande wa JKU wakiwa na pointi 48.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Zimamoto, Mohmmed Ali Hilali, alisema mipango yake mikubwa ni kuhakikisha anamaliza ligi hiyo akiwa nafasi ya pili, hivyo katika michezo mitano iliyobaki atahakikisha yote anashinda ili kutimiza lengo lake hilo.

"Tumebakisha michezo mitano, michezo hii hatutaki tufanye makosa, tunataka tushinde ili tukae nafasi ya pili na hili litawezekana endapo wachezaji watajituma," alisema huku akiweka wazi kuwa anataka kuanza na ushindi katika mechi yao ya leo dhidi ya Black Sailor.

Katika kufanikisha hilo, aliwataka mashabiki wa Zimamoto kujitokeza kwa wingi katika michezo mitano iliyobakia ili kuongeza hamasa kwa wachezaji kuweza kupambana.

## Netiboli Afrika kupigwa Sauzi

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya Kombe la Afrika ya mchezo wa netiboli, yanatarajiwa kuanza kutimua vumbi Agosti 20 hadi 26, mwaka huu nchini Afrika Kusini, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Chama cha Netiboli Tanzania (Chaneta), Devota Marwa, alisema kwa upande wa Tanzania, timu itakayoshiriki ni Taifa Queens, ambayo hivi karibuni itaingia kambini.

"Kwa sasa tupo kwenye maandalizi ya kutafuta sehemu ya kuweka kambi ili tuanze maandalizi ya mashindano mapema," alisema Marwa.

Aidha, mwenyekiti huyo aliwaomba wadau mbalimbali kujitokeza kuiunga mkono timu hiyo ili ifanikishe mipango yake ya safari.

"Tunaomba wadau mbalimbali watuunge mkono ili tufanikishe safari yetu kuelekea Afrika Kusini, tuna imani tutakwenda kufanya vizuri," alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### POGBA NA MAN UNITED

KLABU ya Juventus itafanya mazungumzo mapya na wawakilishi wa Manchester United na kiungo wa kati wa Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 29. ***(Mirror)***

### HENDERSON AWANIWA




NEWCASTLE inataka kumchukuwa mlinda mlango wa Manchester United na England, Dean Henderson mwenye umri wa miaka 25. ***(Mirror)***

### MBAPPE KUAMUA PSG

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 23, amesema yuko "karibu", kufanya uamuzi juu ya mustakabali wake wa baadaye na atatangaza "hivi karibuni kabisa" baada ya kuhusishwa na uhamisho wa kuondoka Paris St-Germain. ***(Get Football News France)***

### NEVES HUYOOO BARCA



BARCELONA wanakaribia kusaini mkataba na kiungo wa kati wa Wolves na Ureno, Ruben Neves mwenye umri wa miaka 25. ***(Sport)***

### EKITIKE KUMRITHI HAALAND

KLABU ya Newcastle inamtaka mshambuliaji wa Reims, Hugo Ekitike mwenye umri wa miaka 19, lakini Borussia Dortmund pia wanatafakari iwapo watamchukua Mfaransa huyo kuziba nafasi ya Erling Haaland. ***(Fabrizio Romano)***

### POCHETTINO NA PSG



KOCHA wa Paris St-Germain, Mauricio Pochettino, yuko tayari kukutana na rais wa klabu hiyo, Nasser Al-Khelaifi huku kukiwa na tetesi kuhusu hali yake ya baadaye. ***(Marca)***

### LEWANDOWSKI NA BAYERN

RAIS wa heshima wa Bayern Munich, Uli Hoeness ameserma madai ya mshambuliaji, Robert Lewandowski kwamba hatasaini mkataba mpya "yote ni kuhusu fedha" na anaimani raia huyo wa Poland mwenye umri wa miaka 33, atabakia katika klabu hiyo msimu huu.***(Kicker)***

### BELLINGHAM ANUKIA LIVER



LIVERPOOL ipo mstari wa mbele katika kinyang'anyiro cha kumsajili kiungo wa kati wa timu ya vijana wadogo ya Birmingham, Jobe Bellingham mwenye umri wa miaka 16. ***(Mirror)***

### JUVE NA GABRIEL ARSENAL


KLABU ya Arsenal inaangalia uwezekano wa kumuuza Gabriel mwenye umri wa miaka 24 huku Juventus wakiwa na nia na mchezaji huyo. ***(Tuttosport)***

### ERIKSEN AITAKA UEFA



NYOTA wa Denmark, Christian Eriksen, 30, ambaye kwa sasa ana mkataba wa muda mfupi na Brentford, amesema angependa kucheza kwenye Ligi ya mabingwa Ulaya. ***(Viaplay via Football365)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGA A ULAYA



# GUARDIOLA: LIVER NI TIMU BORA NILIYOWAHI KUIONA

## ●●● Dhidi yao huwezi kushinda ligi mwezi mmoja uliopita ama mechi mbili au tatu zilizopita, lazima...

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesema Liverpool ni "mojawapo ya timu bora zaidi ambayo nimeona maishani mwangu" na anafurahi kuwa mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England zinaelekea kumalizika "kwa haki".

**Kikosi cha Guardiola Manchester City kilipambana na kupata sare ya mabao 2-2 dhidi ya West Ham, Jumapili huku Riyad Mahrez akikosa penalti ya dakika za lala salama.**

Inamaanisha kuwa City wanaongoza kwa tofauti ya pointi nne dhidi ya Liverpool, ambao bado wana mechi mbili za kucheza na watahakikisha mbio za kuwania taji hilo zinakwenda kasi mradi tu waepuke kufungwa na Southampton leo Jumanne.

"Niliwaambia wachezaji baada ya mchezo kumalizika tusitegemee tofauti yoyote dhidi ya timu inayopigania kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ambayo ni miongoni mwa timu zilizokamilika ambazo nimezieona katika maisha yangu," alisema Guardiola baada ya mchezo huo.

"Dhidi ya Liverpool hii huwezi kushinda ligi mwezi mmoja uliopita au mechi mbili au tatu zilizopita. Lazima upigane hadi mwisho.

"Nilisema (wachezaji) leo (juzi) usiseme kwa sababu ulifanya vizuri na ni haki dhidi ya mpinzani huyu kufika siku ya mwisho kuamua nani bora, kwa sababu timu zote mbili ni nzuri sana."

Jack Grealish ambaye alitua City msimu uliopita kwa pauni milioni 100, ndiye aliyeisawazishia City kipindi cha pili kwenye Uwanja wa London.

Kiungo huyo wa kati wa England amesema msimu huu ni wakati ambao anausubiria kubeba taji na City.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
SOUTHAMPTON
VERSUS
LIVERPOOL
1 | 6.50
X | 5.12
2 | 1.37

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+ GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa




# MBAPPE KUWEKA WAZI HATIMA YAKE MAPEMA

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe amefichua kuwa atatangaza uamuzi wake kuhusu hatima yake kabla ya kujiunga na timu ya Taifa ya Ufaransa kwa ajili ya mechi za Ligi ya Mataifa ya Ulaya, Uefa Ligi.

Huku mkataba wake na mabingwa wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, Paris Saint-Germain ukitarajiwa kumalizika mwezi ujao, Mbappe amekuwa akihusishwa vikali na kuhamia Real Madrid.

Ripoti zinazokinzana zimeeleza PSG wana uhakika wa kumpa mkataba mpya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, wakati uongozi wa Bernabeu ukiwa na uhakika wa kumvutia nchini Hispania.

Mbappe, mshindi wa Kombe la Dunia mwaka 2018, amefunga mabao 36 na kutoa pasi za mwisho 21 kwa PSG msimu huu, na kuwawezesha kunyakua taji la 10 la Ligue 1 katika historia ya klabu hiyo.

Jumla ya mabao 57 aliyochangia msimu huu yanaweza tu kuboreshwa na mchezaji mwenzake wa kimataifa Karim Benzema (59), miongoni mwa wachezaji katika ligi tano bora za Ulaya msimu huu.

Akizungumza katika hafla ya kila mwaka ya tuzo za Union Nationale des Footballeurs Professionels (UNFP), jijini Paris ambapo alitajwa kuwa mchezaji bora wa Ligi Kuu Ufaransa kwa mara ya tatu katika kipindi cha miaka minne, Mbappe alifichua kuwa hivi karibuni ataweka wazi kuhusu hatima yake.

"Nilifanya kosa hili miaka mitatu iliyopita. Ninataka kushiriki katika sherehe, na si kutafuta utukufu," alisema Mbappe.

"Tutajua haraka sana, karibu imekwisha. Chaguo langu limefanywa, ndiyo, karibu."

"Nitatangaza rasmi uamuzi wangu kuhusu siku zijazo kabla ya kujiunga na timu ya taifa ya Ufaransa Juni."




## Suarez kuondoka Atletico

**MADRID,** Hispania

LUIS Suarez ataondoka Atletico Madrid mwishoni mwa msimu huu baada ya kukaa kwa miaka miwili pale Wanda Metropolitano, miamba hao wa LaLiga wametangaza Jumapili.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Barcelona na Liverpool, Suarez alitoa cheche msimu uliopita na kuisaidia timu ya Diego Simeone kutwaa ubingwa wa LaLiga.

Hiyo ilikuwa kampeni yake ya kwanza akiwa na Atletico baada ya kuhama kutoka Barcelona, na alimaliza akiwa na mabao 21 katika mechi 32 za ligi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, hajawa kwenye kiwango bora kama msimu uliopita.

Uthibitisho ulikuja pale Atletico iliposema kabla ya mechi ya Jumapili dhidi ya Sevilla kwamba, utakuwa mchezo wa mwisho wa nyumbani kwa Suarez na Hector Herrera, ambao Machi walikubali kuhamia Houston Dynamo mwishoni mwa msimu.

Atletico walisema katika taarifa yao kwenye Twitter: "Mwishoni mwa mchezo, Wanda Metropolitano watatoa heshima kwa Luis Suarez na Hector Herrera, ambao wanaaga familia ya Wekundu na Weupe leo (juzi)."

CHEZA USHINDE KASINO
JISAJILI CHEZA SHINDA



# MASSAWE WA KILUVYA ASHINDA BILIONI 1.2/- JACKPOT SPORTPESA

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Michezo na Burudani ya SportPesa imemtangaza mshindi wa Jackpot ya shilingi 1,255,316,060, ambaye ni Florian Valerian Massawe (36), kutoka Kiluvya mkoani Pwani.

**Florian ambaye ni fundi makenika amekuwa bilionea wa kwanza wa SportPesa baada ya kubashiri kwa usahihi mechi zote 13 za Jackpot za wiki iliyopita.**

Akimtangaza mshindi huyo wa awamu ya nane, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi SportPesa, Tarimba Abbas, alianza kwa kumpongeza Florian kwa ushindi wake na kuwa bilionea.

"Ni furaha yangu kubwa sana kwa niaba ya kampuni kumtangaza kwenu Florian Valerian Massawe kuwa ni mshindi rasmi wa Jackpot yetu akiwa amejishindia bilioni 1.2".

"Ikiwa ni takriban miezi 14 tangu kumtangaza mshindi wa mwisho wa Jackpot ambapo alipelekea Jackpot yetu kukua kwa kasi mpaka kufikia bilioni moja ikiwa ni mara ya kwanza kwenye historia ya Tanzania, lakini leo kwa furaha kubwa lile jambo letu limetimia.

"Hili ni jambo la kihistoria kwa kampuni ya kubashiri kumtangaza mshindi wa kiasi kikubwa (bilioni 1.2) kwenye sekta ya michezo ya kubashiri na kwenda kukabidhiwa pesa yake," Tarimba alisema na kuongeza;

"Fedha hizi alizoshinda tayari zipo kwenye akaunti yake ya SportPesa na tunafuata utaratibu ili kuhakikisha tunamkabidhi maana malipo yetu sisi ni papo hapo baada ya kuibuka mshindi."

Ni miaka mitano sasa tangu kuanzishwa kwa Kampuni ya SportPesa ikiwa imetangaza jumla ya washindi nane wa Jackpot.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi SportPesa, Tarimba Abbas, akimtangaza mshindi wa Jackpot ya wiki iliyopita, Florian Valerian Massawe, ambaye amejishindia Sh. bilioni 1.2 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi zote 13. **PICHA: SPORTPESA**

# *Kocha Polisi alia na mastraika*



**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini, amelalamika kuwa mastraika wake wanamwangusha kwenye upande wa kufunga mabao kwani kila mechi wanatengeneza nafasi nyingi ambazo hazitumiwi vizuri.

Alisema hayo juzi baada ya kumalizika kwa mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya timu yake ikiwa ugenini, Uwanja wa Sokoine Mbeya dhidi ya Mbeya City na kutoka suluhu.

Alisema kwa muda mrefu kwenye kikosi chake kumekuwa na matatizo ya ufungaji mabao, kitu ambacho kinasababisha timu yake ipate matokeo ya kusuasua.

"Mechi ilikuwa nzuri, lengo lilikuwa ni pointi tatu, lakini tumepata moja, bado hatujakata tamaa, tunarudi nyumbani, ila tunatengeneza nafasi nyingi, lakini safu yangu ya ushambuliaji haijakaa sawa.

"Kwenye mechi kama hizi usitegemee kupata nafasi sita kwa mchezo mmoja, sasa unapopata hata moja utumie, hata dakika ya 89 tumepata nafasi lakini straika wangu akakosa, hivyo tatizo langu kubwa linaloniangusha ni safu ya ushambuliaji," alilalamika kocha huyo ambaye timu yake imeporomoka hadi nafasi ya 12 ikiwa na pointi 27.

Kwa upande wa wenyeji, Kocha Mkuu, Mganda Mathias Lule, alisema wapinzani wao waliingia kwa lengo la kutafuta sare tu.

"Polisi Tanzania wao waliingia kutafuta sare, wakakaa nyuma kwa muda mrefu, sisi tulitaka kushinda, wao walikuwa nyuma ya mpira, hivyo kuwapa kazi kubwa washezaji wangu kuwafungua," alisema.

Matokeo hayo yanaiweka Mbeya City kwenye nafasi ya nne ya msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa na pointi 32.

SPORTPESA APP
PAKUA APP YETU,
BET LEO UWE MILIONEA

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMANNE - 17/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1411 | Daejeon Citizen vs Busan I Park | 1.57 | 3.74 | 5.05 |
| 13:00 | 1773 | Suwon Samsung vs Sangju Sangmu | 2.73 | 3.02 | 2.48 |
| 13:00 | 2967 | Jeonnam Dragons vs Anyang | 2.71 | 3.00 | 2.52 |
| 13:00 | 4821 | Bahir Dar Kenema FC vs Adama City FC | 2.14 | 2.68 | 3.85 |
| 13:30 | 4183 | Seoul E Land vs Gimpo Citizen | 1.61 | 3.55 | 5.05 |
| 13:30 | 5081 | Incheon Utd vs Daegu | 2.53 | 3.02 | 2.68 |
| 14:00 | 2902 | Mbeya Kwanza FC vs Geita Gold FC | 2.48 | 2.67 | 3.11 |
| 15:15 | 1239 | Sarawak vs Kuala Lumpur | 3.37 | 3.37 | 1.97 |
| 15:15 | 2167 | Projek Fam vs Msn-Uitm FC | 3.51 | 3.22 | 1.98 |
| 16:00 | 1100 | Shukura vs FC Samtredia | 1.56 | 3.83 | 5.04 |
| 16:00 | 2661 | Arba Minch Kenema vs Hawassa Kenema SC | 2.73 | 2.78 | 2.68 |
| 16:00 | 4210 | Penang vs Sabah | 1.97 | 3.30 | 3.45 |
| 16:00 | 4405 | Biashara United vs Namungo | 2.26 | 2.63 | 3.60 |
| 16:00 | 4481 | FC Spaeri vs WIT Georgia | 2.02 | 3.30 | 3.30 |
| 16:00 | 4653 | Metalurgi R vs Gareji | 2.50 | 3.30 | 2.70 |
| 16:00 | 4985 | Kedah vs Negeri Sembilan | 1.48 | 4.18 | 5.44 |
| 17:00 | 2456 | Navbahor Namangan vs Neftchi Fargona | 1.43 | 3.99 | 6.62 |
| 17:00 | 2505 | Metallurg Bekabad vs Dinamo Samarqand | 1.66 | 3.44 | 4.85 |
| 17:00 | 2990 | Nasaf Qarshi vs Qizilqum | 1.50 | 4.00 | 6.40 |
| 17:00 | 4630 | El Gouna vs Misr Lel Makasa | 2.06 | 3.08 | 3.78 |
| 17:15 | 1297 | Al Dhafra vs Shabab AL Ahli Dubai Club | 2.78 | 3.32 | 2.28 |
| 17:15 | 3607 | Emirates Club vs AL Urooba | 2.58 | 3.70 | 2.26 |
| 17:15 | 4795 | Al Wasl Dubai vs Ajman Club | 1.59 | 3.97 | 4.56 |
| 18:00 | 1929 | US Monastir vs CS Sfaxien | 2.78 | 2.54 | 2.88 |
| 18:00 | 2056 | Haka vs Seinajoen JK | 2.31 | 2.97 | 3.02 |
| 18:00 | 2069 | AC Oulu vs KuPS Kuopio | 6.02 | 3.84 | 1.49 |
| 18:00 | 3750 | HJK Helsinki vs Lahti | 1.31 | 4.77 | 7.78 |
| 18:00 | 4802 | Tammeka Tartu vs Tallinna Kalev | 1.47 | 4.27 | 5.44 |
| 19:00 | 5099 | AL Sahel SC vs AL Kawkab | 2.07 | 2.92 | 3.65 |
| 19:05 | 2996 | Alshoulla vs Al Wehda | 3.31 | 2.73 | 2.32 |
| 19:30 | 5397 | Coca Cola vs El Ittihad Alexandria | 2.00 | 2.98 | 4.17 |
| 19:35 | 1178 | Jeddah Club vs AL Khlood | 2.33 | 2.85 | 3.40 |
| 19:35 | 1698 | Ohud Medina vs AL Nahdha | 1.99 | 3.01 | 3.78 |
| 20:00 | 1319 | Baniyas vs Al Sharjah SC | 3.84 | 3.69 | 1.76 |
| 20:00 | 2363 | PAOK vs Panathinaikos | 2.24 | 3.13 | 3.23 |
| 20:00 | 2976 | Alleroed FK vs Herstedoster IC | 1.54 | 4.50 | 5.00 |
| 20:00 | 3649 | PAS Giannina vs Aris Salonica | 4.57 | 3.23 | 1.83 |
| 20:00 | 3726 | Flora Tallinn vs Kuressaare | 1.15 | 6.79 | 11.63 |
| 20:00 | 5155 | AEK Athens vs Olympiakos | 1.98 | 3.34 | 3.69 |
| 20:00 | 5407 | Al Nasr Dubai vs Al Ain | 4.01 | 3.71 | 1.72 |
| 21:00 | 1717 | ADO Den Haag vs FC Eindhoven | 2.13 | 3.58 | 3.03 |
| 21:30 | 1109 | Benevento vs Pisa | 2.11 | 3.28 | 3.33 |
| 21:30 | 2616 | Virtus Entella vs Palermo | 2.28 | 3.08 | 2.98 |
| 21:30 | 3638 | Empoli vs Ukraine | 3.75 | 4.10 | 1.79 |
| 21:30 | 3795 | Monopoli vs Catanzaro | 2.57 | 2.86 | 2.77 |
| 21:30 | 4716 | Feralpisalo vs AC Reggiana | 3.07 | 3.07 | 2.23 |
| 21:45 | 3682 | Nottingham vs Sheffield Utd | 2.20 | 3.17 | 3.22 |
| 21:45 | 4695 | Southampton vs Liverpool | 6.50 | 5.12 | 1.37 |
| 22:00 | 2153 | Zamalek vs Talaea El Gaish | 1.76 | 3.04 | 5.58 |
| 23:00 | 2925 | Llaneros FC vs Chico | 3.00 | 3.00 | 2.48 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumanne Mei 17, 2022
Nipashe



Suarez kuondoka Atletico UKURASA 22

# NABI ATOA SIRI USHINDI YANGA NA AMBUNDO

## ●●● Amtaja pia Mauya na uwanja, Mayele naye alia mabeki kumkamia...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amefunguka kuwa siri ya ushindi dhidi ya Dodoma Jiji ni kupanga asilimia kubwa ya wachezaji wenye uwezo wa kucheza kwenye uwanja ambavyo haviko katika bora.

Akizungumza baada ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya timu hiyo na Dodoma Jiji iliyopigwa Uwanja Jamhuri Dodoma juzi, kushinda mabao 2-0 yaliyofungwa na Dickson Ambundo na la kujifunga kwa kipa Mohamed Yusuph, kocha huyo amesema alipanga kikosi chake kutokana na aina ya uwanja wenyewe, na hilo kwa asilimia kubwa ndilo lililompa matokeo kwa sababu walicheza kama alivyotarajia.

**"Mechi ilikuwa nzuri, tulikwenda kucheza na timu nzuri pia, lakini tulijua changamoto ya uwanja tunaokwenda kucheza, hivyo tuliamua kuchagua wachezaji wanaojua kucheza kwenye viwanja hivi," alisema kocha huyo.**

Baadhi ya wachezaji walioonekana kupangwa kwenye mechi hiyo kutokana na aina ya uwanja huo ni Ambundo aliyefunga bao, Zawadi Mauya ambaye alisababisha bao la pili, Dickson Job, Aboubakar Salum 'Sure Boy' na Bakari Mwamnyeto.

Kuhusu ubingwa, kocha huyo amewataka wachezaji wake wasiufikirie, badala yake wacheze kwa kupambana kama walivyofanya kwenye mechi hiyo ili kutimiza malengo yao.

"Tunapaswa kubaki kushinda mechi badala ya kuufikiria ubingwa, tunatakiwa kuwa makini kwa kushinda mechi mpaka siku ya mwisho, tumeona presha tulioipata kwenye mechi hizi zilizopita, wachezaji wanapaswa kubaki na nguvu ya kupambana kama walivyofanya leo (juzi)," alisema Mtunisia huyo.

Straika wa Yanga, Fiston Mayele, ambaye kwa mechi nne mfululizo hajapata bao, alisema mabeki wamekuwa wakimkamia sana ili asiteteme.

"Mechi zote nikicheza mabeki wananikamia sana, ili Fiston asiteteme, napata shida sana, lakini hii inanipa nguvu ya kuendelea kupambana. Pamoja na yote tunashukuru Mungu kwa kupata ushindi kwenye mechi hii, hata kama sijafunga, lakini najua mabao yatakuja yenyewe, hii ni changamoto ya mpira, muhimu ilikuwa timu ishinde kwa sababu timu inayotafuta ubingwa haiwezi kucheza mechi nne bila kupata ushindi," alisema raia huyo wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Naye Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji, Masoud Djuma amesema aliingia kwa ajili ya kuzuia na kufanya mashambulizi ya kushtukiza, lakini kwa bahati mbaya alikutana na timu kubwa yenye wachezaji wenye uwezo mkubwa kuliko wa kwake.

"Nilikuja kukaba na kufanya mashambulizi ya kushtukiza, lakini timu kubwa ni timu kubwa tu, ina kila kitu, wachezaji wazuri, benchi la ufundi pana, ninachoshukuru tumepambana na hawakupata mechi rahisi. Bado tunapambana, ukiondoa Simba na Yanga timu zote zinaweza kushuka, sasa naangalia mechi ijayo dhidi ya Coastal Union ambayo tunakwenda Tanga," alisema raia huyo wa Burundi.

Yanga imefikisha pointi 60 ikiendelea kukaa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo, ikibakisha mechi sita tu kukamilisha michezo 30 ya msimu huu, lakini inaukaribia ubingwa ambao iliupoteza misimu minne iliyopita.



Kiungo wa Simba, Sadio Kanouté, ambaye amerejea akitokea chumba cha majeruhi tayari kwa ajili ya mechi ya kesho dhidi ya Azam FC. **PICHA: MAKTABA**

# Pablo na hesabu kuvuna pointi 21

**Na Saada Akida**

WAKATI kesho akiwa na mechi ngumu 'Mzizima Dabi' ugenini, dhidi ya Azam FC, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco, amesema hesabu zake zimebaki kwenye michezo saba ambayo watavuna pointi 21 ili kuongeza presha kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Bara na watahitaji kuendelea kushinda bila kuitazama Yanga.

Simba ipo nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 49, 11 nyuma ya vinara Yanga waliopo mchezo mmoja mbele baada ya kushuka dimbani mara 24.

Michezi ambayo Simba imebakiza ni dhidi ya Azam FC, Geita Gold, Tanzania Prisons, Mbeya Kwanza (ugenini) na KMC, Mbeya City na Mtibwa Sugar itakazokuwa nyumbani.

Akizungumza na gazeti hili jana, Pablo alisema amepanga kushinda mechi zote saba zilizosalia ili kufikisha pointi 70 na akiiombea Yanga ipoteze na kutoka sare ili kufikia malengo yao ya kutetea ubingwa huo.

Alisema ili kuhakikisha hilo linatimia wanapaswa kusaka pointi zote 21 katika michezo saba wakati huu ambao ataendelea kuwapa nafasi wachezaji wake wote kuepuka uchovu kwa baadhi yao kutokana na ratiba kuwa na muda mfupi wa mapumziko.

"Bado hatujatoka katika mbio za kutetea ubingwa, tuna nafasi kubwa ya kuhakikisha tunashinda mechi zote saba zilizosalia bila kuangalia wapinzani wetu (Yanga) wanafanya nini, lakini wakipoteza mechi tatu na sare mbili watakuwa wanajiondoa katika mbio za ubingwa," alisema kocha huyo.

Alisema kwa sasa anahitaji kumpa kila mchezaji nafasi kwa sababu mechi iliyopita waliwakosa wachezaji wengi waliokuwa nje wakiuguza majeraha.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >